tigo pesa SportPesa
MAOKOTO Deilee!
WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



**Waziri:** Utoroshaji madini umerudi, mtaona sura yangu halisi

UKURASA 3


Ukurasa 12 Vijana wakizibaini tamu, chungu za mitandao ya kijamii watafanikiwa
Ukurasa 13 Ufugaji unavyowatoa vijana baada VETA kuwaanzishia program 'spesho'
Nipashe TESA
Jumanne Septemba 12, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Ukurasa 14 Maisha mapya kwenye mwezi ni dhahiri baada ya kuthibitika kuwa maji yapo
ELIMU
NA MARCO MADUHU, SHINYANGA
MWIBA NDOA UTOTONI
Kutumia mabibi harusi feki mbinu inayobuniwa kukwepa rungu la dola
KATA ya Masengwa wilayani Shinyanga ni maarufu si kwa kilimo au maisha bora kwa wanavijiji laa, ila inatikisa anga kwa kukatisha masomo mabinti na kuwaozesha utotoni pia wakiwatumia mabiharusi feki kuficha ukweli.
Mchungaji wa Kanisa la Kipetentekoste PAG Shinyanga, Edward Salamba, akizungumzia vita ya kutokomeza ndoa kwa wasichana wadogo, anaiamsha serikali kwamba katika kudhibiti ndoa hizo za utotoni, wanapaswa kuwa makini sababu jamii imekuwa na mbinu nyingi ikiwamo kuweka mabibi harusi feki ambao wana zaidi ya miaka 18.
Ndoa ya binti wa miaka 15 iliyofungwa Malawi. PICHA: MTANDAO

UKURASA 11

Nipashe
Jumanne Septemba 12, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581431
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# Rais Samia aweka wazi msimamo wake Katiba Mpya

• **Atahadharisha** wanasiasa; wadau walonga ya kwao... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### NIC INSURANCE YAJIVUNIA KULIPA BIMA WATEJA NDANI YA SIKU SABA



NIC Insurance imetangaza mafanikio yake ikieleza kuwa hivi sasa mteja anaweza kulipwa madai ya bima ndani ya siku tatu...

KESI MAUAJI YA DADA WA BILIONEA MSUYA

### Utata wa shahidi sahihi, jaji aweka kiporo hadi kesho

UKURASA 4



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akisalimiana na baadhi ya wanachama wa chama hicho jijini Arusha jana, baada ya kuhojiwa na Jeshi la Polisi. **PICHA:GETRUDE MPEZYA**

# Lissu awashangaa polisi kwa kilichomkuta Arusha

UK. 3

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA LIGI KUU KIMEELEWEKA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Baadhi ya washiriki wa Mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa wakimsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia aweka wazi msimamo Katiba Mpya

**Na Halfan Chusi**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema ni lazima Watanzania waelimishwe, waijue Katiba ya nchi kabla ya kuanza mchakato wa Katiba Mpya.

Vilevile, Mkuu wa Nchi amesisitiza nyaraka hiyo si kwa ajili ya wanasiasa, bali inamhusu kila mwananchi.

Ni ufafanuzi alitoa jana jijini Dar es Salaam, alipozindua Mkutano Maalum wa Baraza la Vyama vya Siasa na Wadau wa Demokrasia Kutathmini Utekelezaji na Mapendekezo ya Kikosi Kazi na Hali ya Siasa nchini.

Alisema: "Wanasiasa tunadhani tuna haki ya kuburuza watu. Tunachokisema sisi (wanasiasa) watu wote wafuate. Tunageuza watu makasuku. Tunataka Katiba Mpya, basi watu wote Katiba Mpya.

"Mwulize 'kifungu gani cha Katiba kinakuudhi?' hajui, au 'unataka nini kibadilike, maana yake tunataka mpya tu, mpya ilete nini?' Unajua ndiyo hivyo, ndio maendeleo.

"Nani kasema maendeleo yanaletwa na kitabu kilichotungwa kikawekwa hapa (anaonyesha)? Kama kuheshimu vitabu tungeheshimu vya dini ndivyo vya kuheshimiwa. Wangapi tunavikiukwa au tunaviheshimu? Huwezi kuheshimu kitabu mpaka ukijue maana yake.

"Hata cha dini huwezi kuheshimu msaafu wako mpaka ujue humo ndani mna nini. Huwezi kuheshimu Bible (Biblia) mpaka ujue humo ndani mna nini, na ndio maana mtu anarandа nayo lakini matendo yake ni tofauti na yaliyomo ndani.

"Kwahiyo, Katiba sio kitabu, bali ni 'morality', 'ethical standards' yaliyoandikwa tumekubaliana Tanzania tunaenda hivi, maadili yetu yatakuwa hivi kila mtu ajue, azitambue halafu tunaweka kwenye kitabu.

"Lakini Katiba iwapo mioyoni ili watu waiamini na iwe ndio itikadi yake kama walivyofanya wenzetu, hawakurupuki. Tuna kazi ya kuwafanya Watanzania waijue hiyo Katiba ni nini. Ukienda kijijini mtu anakuja na Ilani ya CCM anasema ni Katiba.

"Tusiwaburuze Katiba, viongozi wa siasa siyo yetu, ni mali ya Watanzania. Tunachokitaka ni maoni ya Katiba iweje. Nimemwambia Msajili, viongozi wa siasa walete maoni ya ushiriki wao kwenye mchakato wa Katiba kwenye Kikosi Kazi au Kamati itakayoundwa," alisema.

**MIKUTANO YA HADHARA**

Rais Samia pia alisema serikali iliruhusu mikutano ya hadhara ili vyama vya siasa vikue, virudishe wafuasi wao kwa hoja, lakini anashangazwa kuona baadhi yao wametumia mwanya huo kutoa maneno ya kashfa na kuvunja sheria za serikali na kibinadamu.

"Unakuta mtu yuko kwenye jukwaa la siasa, anashindwa kuongea kwa hoja, anaanza kutukana, kukashfu na hata kuchambua dini za watu kwa sababu hana hoja ya kuzungumza.

"Kunapokuwa hakuna cha kukosoa, wanalazimisha kusema jambo, mwisho wa siku wanasema lisilokuwapo. Vyama vya siasa tumieni hiyo fursa, kajijengeni kwa wananchi ili warudi. Tukienda katika uchaguzi, vyama vyote viwe vizuri na vimejipanga kwa hoja.

"Hakuna mtu aliyepewa hati ya kumiliki Tanzania. Hii ni nchi yetu sote, kwamba yeye ndiye mmiliki wa Tanzania! Hata mtoto mdogo akizaliwa ana haki yake. Kwahiyo, hakuna mtu mmoja atakayekuja kusema nchi hii ni ya kwangu na kutulazimisha kufuata anachokitaka yeye," alisema.

Rais Samia alisema watu wametofautiana kiutendaji, lakini tofauti hizo zisitumike kuleta mambo ambayo hayana afya kwa ustawi wa taifa na kuharibu sifa na baraka za kipekee kwa nchi.

"Hakuna aliye juu ya sheria. Ukikosea utawajibishwa. Ajenda yetu kubwa kama Watanzania ni kusimamia amani, mshikamano na umoja kwa maslahi ya taifa letu. Kuna watu wana roho za kutu, wanataka kuona Tanzania ipo kwenye mgogoro kila siku. Hao sio marafiki," alionya.

**UHURU WA MAONI**

Rais Samia pia alisema anaona watu wanavyojieleza kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Anachukua mazuri na ana kikundi maalum ambacho kazi yake ni kuchuja maoni kuchakata na kuyafanyia kazi.

"Hakuna uhuru usio na mipaka na mipaka yetu si tu ya kisheria, hata kibinadamu. Kama ulipata malezi mazuri ukapitishwa kwenye masomo ya dini.

"Kuna mambo huwezi kufanya. Sasa utasikia ooh mama una kifua, unastahimili jamani...! Sasa kama chizi anatoka na nguo, ukimfukuza na utupu wako nani ataonekana chizi?

"Muungwana anajua mipaka yake, lakini sasa unakuta mtu sio muungwana kajikulia huko. Jamani hata ng'ombe, wana utamaduni wao, wengine wameletwa kama jogoo tu kafumba macho, kafumbua kaona jogoo tu hajapitia kwenye malezi ya dini," alisema.

**DEMOKRASIA**

Rais Samia pia alisema serikali imeanza kufanyia kazi mapendekezo ya vyama vya upinzani ili kuimarisha demokrasia, ikiwamo kuruhusu uhuru wa kutoa maoni na kuondoa zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa.

Awali, Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Prof. Ibrahimu Lipumba, aliimwomba Rais kuyafanyia kazi mapendekezo yao walioazimia kwenye mkutano wao uliopita.

Aliyataja maazimio hayo mbele ya Rais kuwa ni pamoja na kuendelezwa mchakato wa Katiba Mpya, kuwekwa viraka kwenye Katiba ya sasa ili kupata tume huru ya uchaguzi, kuruhusu mgombea binafsi, Rais atangazwe mshindi akishinda kwa zaidi ya asilimia 50 ya kura.

Mengine ni matokeo ya uchaguzi wa Rais yahojiwe mahakamani. Jambo ambalo alilipokea na kuagiza maoni hayo yaambatanishwe na yatakayojadiliwa kwenye mkutano huo.

Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, aliomba serikali kuendelea kuandaa mikutano kama hiyo ili kutoa fursa kwa wadau na vyama vya siasa kutatua na kuwasilisha changamoto zao.

**NJE YA MKUTANO**

Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana ya ACT Wazalendo, Abdul Nondo, alizungumzia kauli ya Rais Samia kuhusu Katiba Mpya, alisema muda uliopangwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi (miaka mitatu) ni mirefu. Yafanyike mabadiliko madogo Ili ipatikane tume huru ya uchaguzi mwaka huu.

Alisema pamoja na Rais kusema utatumika muda mwingi kupata Katiba Mpya, wanachohitaji kwa sasa ni mabadiliko madogo yatakayoruhusu tume huru ya uchaguzi wakati mchakato wa Katiba Mpya ukiendelea.

"Kuwe na ratiba ya utekelezaji lini utaanza na mchakato uanze mapema na kuwe na ratiba inayoeleweka. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa usimamiwe na tume huru ya uchaguzi na si Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Sheria ya Jeshi la Polisi ibadilishwe ili tuepukane na adha hii ya askari kuingilia mikutano ya vyama vya siasa na kuvuruga uchaguzi," alishauri.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga alisema kutoa elimu kwa umma ni muhimu, lakini muda wa miaka mitatu ni mirefu sana.

"Elimu kweli ni jambo la muhimu, lakini muda wa miaka mitatu ni mwingi sana. Wangeangalia namna ya kupunguza Ili mchakato huo ukamilike mapema zaidi," alishauri Dk. Anna.



# Lissu awashangaa polisi kwa kilichomkuta Arusha

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu na viongozi wengine waandamizi wa chama hicho, wanaotuhumiwa kufanya mikusanyiko bila kibali na kuzuia polisi kufanya kazi yao wamehojiwa kwa saa nne.

Kabla ya mahojiano hayo na timu ya maofisa upelelezi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Arusha, Lissu na wenzake waliwasili katika Kituo Kikuu cha Polisi Arusha saa 2:30 asubuhi na saa 3:30 walianza kuhojiwa hadi saa 7:30 mchana.

Baadaye Lissu alieleza waandishi wa habari kilichojiri katika mahojiano na maofisa hao wa polisi, akiwa na ufafanuzi:

"Nilikuja Ofisi ya RCO (Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa) kuandika maelezo. Na kwa wale msiojua tuhuma zangu, nilikamatwa jana (juzi) asubuhi, nikituhumiwa kuziba barabara, wakati nilikuta barabara ilishazibwa na watu wasiokuwa na 'uniform' (sare).

"Nikawauliza, 'ninyi ni kina nani?' Wakasema wao ni polisi. Nilipowauliza vitambulisho, wakasema 'wewe unakwenda Ngorongoro bila kibali'. Hapo ndipo kosa lilianzia. Lakini niliambiwa kosa langu ni kukusanyika bila kibali.

"Ngorongoro si gereza, wala mahali ambapo watu hawaruhusiwi kuingia. Hivyo, tutakwenda na tutazungumza na watu wa Ngorongoro, vinginevyo...

"Ninashangazwa na polisi kusema niliziba barabara, wakati wao ndio waliweka kizuizi na walipotaka kuwapiga watu tuliokuwa nao, nikawaambia wakae chini."

Akaendelea: "Vibali vinatolewa na Mamlaka ya Ngorongoro (NCAA), na si polisi. Iweje Jeshi la Polisi litake kuchukue vibali kwao? Kuna kitu gani wanaficha?

"Mikutano ya Ngorongoro ilikuwa ya kumalizia, maana tulishafanya miwili, ila hapa tulikuwa tunakwenda kumalizia. Hatuwezi kurudishwa nyuma, wala kunyimwa kufanya mikutano; hivyo tunakwenda kupumzika na tutarudi kuendelea na mikutano yetu.

"Lengo la kutuzuia ni ili tusiende Ngorongoro, maana wanajua tukienda Ngorongoro, kazi ya kuondoa wakazi 100,000 na ushee haitakuwa ya kawaida, lakini tunakwenda kujichaji, tutarudi na tutakwenda kila mahali kufanya mikutano."

Lissu aliongeza kuwa yuko nje kwa dhamana. Baada ya mwezi mmoja, atarejea polisi kama alivyotakiwa na jeshi hilo, anasubiri hatua nyingine ziendelee kama zipo.

Mtaalamu huyo wa sheria alikamatwa wilayani Karatu, mkoani Arusha saa nne asubuhi ya Septemba 10 mwaka huu, akiwa na viongozi wengine katika Hoteli ya Ngorongoro Coffee, wakijiandaa kwa ajili ya mkutano wa hadhara ambao ulipangwa kufanyika katika Viwanja wa Mazingira Bora.

Baada ya kutiwa mbaroni, Lissu na wenzake walisafirishwa kutoka Karatu hadi jijini Arusha, ambako alichiwa kwa dhamana na wenzake usiku.

Viongozi wengine waandamizi wa CHADEMA waliokamatwa sambamba na Lissu ni Katibu wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA), Catherine Ruge, Mjumbe wa Kamati Kuu, Suzan Kiwanga, Twaha Mwaipaya, walinzi wa Lissu na watu wengine ambao hawakutajwa kwa majina.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Tumaini Mafie**

# Waziri Mavunde: Utoroshaji madini umerudi, mtaona sura yangu halisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, amesema atawashughulikia watoroshaji wa madini bila kuangalia sura wala cheo cha mtu.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa wachimbaji wadogo wa madini waliopo chini ya Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Wadogo Tanzania (FEMATA), Mavunde alisema anafahamu kuna tatizo la utoroshaji wa madini limeanza kuibuka, atahakikisha anasimamia sheria ipasavyo bila kuangalia sura ya mtu.

"Hata kama mnanifahamu mimi ni mtoto wenu (amewahi kuwa Mtendaji Mkuu wa Femata), lakini tukifika huko nitasimamia sheria inavyoelekeza na sitasita kuchukua hatua kwa watakaobainika."

"Nitasikiliza kushauriana namna ya kudhibiti utoroshaji wa madini na tutakuwa wakali sana eneo hili, mimi nimesoma seminari na nilitaka kuwa padre, lakini sikufikia hatua hiyo, msinione nina uso wa kipaimara na sauti ya upole, lakini nina sura ya tofauti kwenye suala la utoroshaji wa madini nitakuwa mkali," alionya.

Alisema moja ya mtihani mkubwa alionao kwenye wizara hiyo ni kufikia lengo la kukusanya maduhuli ya Shilingi trilioni moja kwa mwaka 2023/24.

Kuhusu mwelekeo wa wizara hiyo, Mavunde alisema amekuja na dira ya madini ni maisha na utajiri mwaka 2030 inayolenga kuweka nguvu kwenye utafiti.

"Nataka ikifika mwaka 2030 nchi yetu iwe na taarifa za kijiolojia kwa maeneo yote ambayo hakuna taarifa zake, hadi sasa eneo lililofanyiwa utafiti wa kina la madini ni asilimia 16 kwenye nchi yetu ina ukubwa wa kilomita za mraba 900,000," alisema.

Alisema ili kufikia lengo hilo mkakati wake ni kuijengea uwezo Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ili kufanya utafiti wa kina wa kisasa wa kupiga picha nchi nzima na kuonesha kila eneo lina madini gani.

Alifafanua kuwa madini ni sayansi hakuna njia ya mkato ili kufanikiwa lazima uwe na taarifa zitakazochochea sekta hiyo. Aliipa siku 30 GST kuwasilisha andiko la kwenda kuomba fedha Wizara ya Fedha litakaloeleza kiwango kinachohitajika kufanya kazi hiyo na manufaa ambayo serikali itayapata.

Alisema hakuna mgogoro wowote atakaousikiliza kabla haujafikia ofisi za mkoa na kuwa vifikiriwe vitu vikubwa vya kujenga nchi na migogoro inayotokana na kutokuwa na taarifa.

Aliahidi kushughulikia kero zilizobainishwa na wachimbaji ikiwamo kushirikiana na Benki Kuu (BoT) kuwawezesha kupata mitaji ili viwanda vya usafishaji dhahabu vipate malighafi.

Rais wa Femata, John Bina, alisema wataendelea kushirikiana na serikali kudhibiti utoroshaji wa madini huku akiomba tozo na ushuru kwenye halmashauri zipangwe kwa kushirikishwa ili kuondoa tatizo la bei kubwa zinazosababisha hali hiyo.

"Kadirio kubwa la kodi linalofanywa na halmashauri ni tishio kuchochea utoroshaji madini, lengo la kupunguza utoroshaji ni kutokuwa na kodi kubwa ili serikali ipate mapato yake na wachimbaji wanufaike," alisema.

"Kuhusu kushuka bei ya Tanzanite tunaomba waziri kuchukua kwa umuhimu wake ili kuhakikisha tunasaidia madini haya ambayo ni pekee."

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Kati Tanzania (CHAMATA), Jeremia Kituyo, aliahidi kutoa ushirikiano wa kudhibiti utoroshaji wa madini kwa kutoa taarifa mchana na usiku na watawasilisha mapendekezo kwa waziri ili kuwashughulikia.

Aliomba madini ya Tanzanite yaruhusiwe kwenda kwenye minada ili iwe biashara nzuri na kuongeza kodi.


HELD UNDER THE PATRONAGE OF HON. DR. DOTO MASHAKA BITEKO (MP), DEPUTY PRIME MINISTER AND MINISTER FOR ENERGY, MINISTRY OF ENERGY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

ENDORSED BY MINISTRY OF ENERGY

Tanzania Energy Congress

20 - 21 September 2023 | Dar Es Salaam, Tanzania

INVESTING IN TANZANIA'S SUSTAINABLE ENERGY ECONOMY

WITH THANKS TO OUR 2023 SPONSORS & PARTNERS TO DATE

DIAMOND SPONSOR: PANAFRICAN ENERGY an Orca Company

PLATINUM SPONSOR: equinor

SILVER SPONSORS: East African Crude Oil Pipeline, TotalEnergies

BRONZE SPONSORS: AGL, CRDB Bank, Maurel & Prom, Neway, NMB, Oryx Energies, PBZ Bank, slb

ENERGY TRANSITION PARTNER: Songas | COUNTRY PARTNER: Oman JSRS eMarketplace | KNOWLEDGE PARTNER: Hawilti | ICT PARTNER: tigo business | BRANDING PARTNER: ZO

SUPPORTING PARTNERS

ORGANISED BY dmg events

BOOK YOUR DELEGATE PASS TODAY

Contact JAYSON ESTRADA on +255755030622 or Email: info@tanzaniaenergycongress.com

tanzaniaenergycongress.com #TanzaniaEnergyCongress

217593902




Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (wa pili kushoto), akizungumza na Mkurugenzi na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP), Sarah Gordon-Gibson, jana kwenye hafla ya kuzindua mabehewa yenye jokofu ya Shirika la Reli nchini (TRC), yatakayotumika kusafirishia mazao ya mboga na matunda. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

### KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Utata wa shahidi sahihi, Jaji alaza kiporo hadi kesho

**Na Grace Gurisha**

WAKILI wa Utetezi, Nehemiah Nkoko katika kesi ya mauaji ya dada wa marehemu Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', Aneth Msuya, amedai kuwa mtu aliyetakiwa kuzungumzia taarifa ya awali ya siri ya Jeshi la Polisi ya tukio hilo kuwa ni feki au la ni SP Richard Mwaisemba na siyo mtunza nyaraka.

Nkoko alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, wakati akimuuliza maswali ya dodoso shahidi namba 23 wa upande wa mashtaka, Sajenti Obadia Mwarukuta, kutoka Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, mkoani Dodoma.

Sajenti Mwarukuta mwaka 2016 alikuwa Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Dar es Salaam, Kitengo cha Kumbukumbu cha Makosa ya Jinai, akiwa anatunza nyaraka mbalimbali zikiwamo hizo (first crime report), mahojiano yalikuwa kama ifuatavyo:

**Nkoko:** Shahidi najua unavifahamu vizuri kielelezo PE 17 na DE III kwa sababu umekuwa navyo hapa mahakamani kwa muda mrefu sana.

**Shahidi:** Nakifahamu vizuri kielelezo kimoja tu cha upande wa mashtaka PE 17 kingine sijui kwa sababu sijakipokea mimi.

**Nkoko:** Ukiangalia kielelezo PE 17 na DE III mengi yaliyokuwapo katika vielelezo hivyo yanafanana yaani hayana tofauti.

**Shahidi:** Hapana siyo yote ni baadhi.

**Nkoko:** Shahidi ni lini uliwahi kukifanyia kazi hadi kukizungumzia kielelezo PE 17.

**Shahidi:** Sikukiandika mimi kielelezo hiki, lakini kililetwa ofisini.

**Nkoko:** Shahidi utakubaliana na mimi kwamba kielelezo hiki hakina mahusiano yoyote na wewe.

**Shahidi:** Ukisema kukiandaa sijakiandaa mimi, ila kuhusu mahusiano, nina mahusiano nacho kwa sababu yeye ndiyo alikipokea ofisini na kukitunza.

**Nkoko:** Wewe huna nafasi ya kulizungumzia hili.

**Shahidi:** Siyo kweli.

**Nkoko:** Ulikuwapo wakati taarifa hizo za awali zinapatikana?

**Shahidi:** Hizi taarifa zililetwa ofisini kwetu.

**Nkoko:** Haya ulikuwapo eneo la tukio?

**Shahidi:** Siku ya tukio sikuwapo.

**Nkoko:** Oh! Kukuwapo eh, na siku wanajaza hizo taarifa.

**Shahidi:** Siku ambayo taarifa zinajazwa kwenye kielelezo PE 17 sikuwepo, lakini kilichoandikwa humu nakijua.

**Nkoko:** Kama ni hivyo, tuelezee upelelezi wa tukio hili ulivyofanyika kwenye hii kesi.

**Shahidi:** Mimi nimekuja hapa kuzungumzia nyaraka na sio kuzungumzia masuala ya upelelezi wa kesi hii.

**Nkoko:** Kwa hiyo nyaraka hii sio sehemu ya upelelezi wa hii kesi?

**Shahidi:** Sijui.

Nkoko: Shahidi vielelezo vyote hivi viwili vinamzungumzia mtu mmoja SP Richard Mwaisemba, soma sehemu iliyoandikwa mlalamikaji.

**Shahidi:** DE III inamwelezea Richard D Mwaisemba SP na PE 17 kinamwelezea Richard Mwasemba SP.

**Nkoko:** Utakubaliana na mimi kwamba Mwaisemba ambaye kwa kipindi hicho ndiye alikuwa Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Kigamboni.

**Shahidi:** Ni kweli.

**Nkoko:** Utakubaliana na mimi sasa kwamba SP Richard Mwaisemba peke yake ndiyo aliyetakiwa kusema kama nyaraka hii ni halali au siyo halali na siyo wewe?

**Shahidi:** Yeye aliifanyia kazi PE 17.

**Nkoko:** Utakubaliana na mimi kwamba Mwaisemba tu ndiye anayeweza kuzungumzia kinaga ubaga kuhusu kielelezo PE 17.

**Shahidi:** Sikubaliani na wewe.

Nkoko: Wewe na Mwaisemba nani bosi.

**Shahidi:** Mwaisemba ni bosi wangu.

**Nkoko:** Unajua hati (mwandiko) wa Mwasemba.

**Shahidi:** Siufahamu.

**Nkoko:** Kwa hiyo hiki kielelezo PE 17 unaweza kusema kimejazwa na Mwaisemba.

**Shahidi:** Aliyeijaza hiyo fomu siyo Mwaisemba.

**Nkoko:** Kwa hiyo unataka kutuambia mwandiko wake unaujua.

**Shahidi:** Mwandiko wake siujui, lakini najua nani aliyejaza hiyo fomu.

Wakati shahidi huyo, akijibu maswali ya ufafanuzi kutoka kwa Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, alidai kuwa siku ambayo jaji amesema katika mwenendo wa kesi hakuna sehemu aliyosikia kuwa SP Mwaisemba aliomba kutoka kielelezo DE III.

Pia alidai kuwa kielelezo hicho hakijatolewa na shahidi wa upande wa mashtaka kama kingekuwa kimetolewa na SP Mwaisemba basi asingeleta mahakamani nakala angeleta nyaraka halisi.

Baada ya ufafanuzi wa maswali hayo, Wakili Kimweri aliomba ahirisho la kesi hiyo hadi Jumatano kutokana na mashahidi aliowategemea kutowapata kwa wakati kwa kuwa wanatoka mikoani.

"Tunaogopa kuiomba mahakama kwamba tuendelee leo kwa sababu hatujui hawa mashahidi tutawapata kwa muda gani kwa hii leo, tunaomba mahakama iridhie na itoe amri ya kuendelea kwa kesi hii kesho kutwa," alidai.

Mawakili wa upande wa utetezi, Kibatala na Nkoko hawakuwa na pingamizi.

Jaji Kakolaki alisema kutokana na sababu zilizotolewa na upande wa mashtaka, analazimika kuahirisha shauri hilo hadi Septemba kesho saa tatu asubuhi.

Katika kesi hiyo, Miriam Mrita ambaye ni mshtakiwa wa kwanza wa mauaji ya wifi yake, Aneth aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kukiri kuhusika na mauaji hayo, katika maelezo yake ya onyo. Mshtakiwa mwingine ni Revocatus Muyela.

# TAMISEMI, kampuni ya tumbaku Japan waingia makubaliano

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameshuhudia utiaji saini wa mkataba kati ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Kampuni ya Tumbaku ya Japan (JT Group) utakayoiwezesha kampuni hiyo kuendelea kutoa huduma za kijamii katika maeneo inayonunua zao la hilo nchini.

Mkataba huo wa miaka mitatu wenye thamani ya Sh. bilioni 3.2, utaiwezesha kampuni hiyo kutoa huduma hizo katika sekta za afya, elimu, maji na uwezeshaji wananchi kiuchumi kwenye maeneo hayo.

Majaliwa alishuhudia utiaji saini wa makubaliano hayo jana katika ofisi ndogo ya Waziri Mkuu iliyoko Magogoni jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya hafla hiyo, Majaliwa alisema hatua hiyo ni matokeo ya mazungumzo kati yake na kampuni hiyo wakati wa ziara yake Japan Septemba mwaka jana na Mkutano wa TICAD 8 uliofanyika Tunisia Agosti mwaka jana.

"Wanataka watumie faida wanayoipata nchini kutokana na biashara yao kuweza kuisaidia jamii, wameamua kuiweka kwenye utaratibu wa kuwa na makubaliano kati yao na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, tayari wameshajenga shule ya wasichana kule Urambo, Tabora, wameshajenga zahanati Uyui, pia wamedhamini vijana kwenye masomo," alisema.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wadau wanaoshirikiana nao, wanakuwa na michango ya maendeleo katika huduma za jamii kwenye maeneo wanakotoa huduma.

Alisema kupitia mkataba huo, kampuni ya JT Group itajenga vituo vya kutolea huduma za afya, shule ya wasichana ya kulala katika moja ya halmashauri wanayozalisha tumbaku.

Pia wataweka miundombinu ya maji safi ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo kwenye maeneo wanayouza tumbaku.

"Kampuni imetoa ajira zaidi ya 450 kwa Watanzania kwenye maeneo wanayonunua tumbaku," alisema.

Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya JT Group, Masamichi Terabatake, alisema kampuni ya JP Group inanunua tumbaku ya kijani katika nchi takribani 35 na Tanzania ni miongoni mwa nchi tano zinazozalisha kwa wingi. Alipongeza Tanzania kwa kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara.

Mpaka sasa kampuni hiyo imeshajenga kituo cha afya huko Uyui mkoani Tabora, shule ya sekondari ya wanawake wilayani Urambo, maeneo ya kuchotea maji na kuendesha programu mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

# Silaa ataka mradi NHC Kawe 711 uliosimama miaka 7 uanze Oktoba



**Na Beatrice Moses**

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa ameagiza ujenzi wa mradi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Kawe 711, uliosimama kwa miaka saba, uanze Oktoba, mwaka huu.

Akizungumza jana wakati wa ziara ya kutembelea miradi ya NHC, alisema ujenzi wa mradi huo umesimama kwa muda mrefu jambo ambalo siyo sahihi na hasara kwa serikali.

Alisema hasara iliyopatikana hadi sasa ni kumlipa mkandarasi gharama za kuuchelewesha mradi huo ulioanza 2017 na riba ya mkopo ambao awali ulitarajiwa kugharimu Sh. bilioni 107.

Kuhusu ujenzi wa mradi wa Samia Housing Scheme wenye nyumba 560, alisema kasi yake inaridhisha na nyumba zimeshauzwa kwa asilimia 88 huku wateja wakiendelea kulipia.

"Mradi wa Samia Housing Scheme usiishie Dar es Salaam, upelekwe kwenye mikoa mingine nao wanufaike, uhitaji wa nyumba za NHC ni mkubwa," alisema.

Aidha, aliutaka uongozi wa NHC kufungua wigo wa kupata mtaji wa miradi yake, ikiwamo kuingia ubia badala ya kutegemea mtaji wake wa ndani au mkopo.

Kuhusu mradi wa Morocco Square, Silaa alisema umekamikia kwa asilimia 98 ukiwa na majengo ya biashara, hoteli na makazi ya nyumba 100.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdallah, alishukuru ushirikiano wanao upata kutoka serikalini katika kutimiza majukumu yao ya kufanikisha ujenzi wa makazi na maeneo ya biashara. Kuhusu mradi wa Kawe 711, alisema imefanyika tathmini kujua kiasi cha hasara kwa miaka saba tangu mradi usimamishwe.

"Mradi huu una mita za mraba 10,000 za biashara, nyumba 440 na eneo kubwa la mazoezi, ni mradi wa kisasa iwapo utakamilika utaleta maendeleo kibiashara, makazi na afya," alisema Mkurugenzi Abdallah.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2017/18, ilionesha NHC lipo hatarini kupata hasara ya mabilioni ya fedha kutokana na miradi yake kadhaa iliyosimama.

Miradi hiyo ni wa nyumba wa Golden Premier Residence (711-2) uliopo Kawe, Dar es Salaam Kitalu Na. 711/2 Oktoba 16, 2013 ambao ulitajwa kuwa haundelei vizuri.

Ripoti hiyo ilibainisha kuwa kama NHC ingekosa kibali cha kukopa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango (sasa Wizara ya Fedha) kutokana na kufikia ukomo wake wa kukopa, itapaswa kuwalipa wakandarasi Sh. bilioni 99.99 kwa kuvunja mikataba.

Aidha, serikali iliruhusu NHC kukopa Sh. bilioni 173 ili kukamilisha ujenzi wa miradi iliyokwama ikiwamo Morocco Square na Kawe 711.

## NIC Insurance yajivunia kulipa bima wateja ndani ya siku saba

**Na Restuta James**

NIC Insurance imetangaza mafanikio yake ikieleza kuwa hivi sasa mteja anaweza kulipwa madai ya bima ndani ya siku tatu hadi saba, kutoka wastani wa siku 45 mwaka 2019.

Aidha, imesema thamani ya shirika imeongezeka kutoka mali zenye thamani ya Sh. bilioni 350.36 mwaka 2019/20 hadi Sh. bilioni 423.9, mwaka jana.

Hayo yalielezwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa NIC Insurance, Dk. Elirehema Doriye, alipokuwa akizungumza na wahariri na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya shirika hilo.

Alisema shirika hilo linafanyakazi kwa kuzingatia viwango vya ubora wa kimataifa hivyo mteja akiwasilisha madai anahudumiwa ndani ya muda mfupi.

"Vile vile, mteja anaweza kukata bima kwa kutumia application yetu ya NIC kiganjani na kufungua madai kwenye mfumo. Tumepunguza sana matumizi ya karatasi ili kuweka uwazi, weledi na uwajibikaji katika utendaji wetu," alisema.

Dk. Doriye alisema mwaka 2020/2021, asilimia 13 ya mapato ya shirika hilo yalisajiliwa kidijitali kutokana na maboresho ya mifumo ya Teknolojia ya Habari (TEHAMA).

"Tuliwatafuta wateja wetu waliokuwa wakitudai tangu mwaka 1994 na tumewalipa wote, naweza kusema kwamba NIC hatuna hata mteja mmoja anayetudai," alisema.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu, shirika hilo limelipa Sh. bilioni 73.97 za wateja kwa bima za maisha, mali na ajali ambayo alisema yamelipwa ndani ya siku saba.

Kuhusu faida, alisema mwaka jana shirika lilitoa gawio la Shilingi bilioni mbili kwa serikali na kulipa kodi ya Sh. bilioni 15.1.

"Mali zimekua kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, kutoka mali zenye thamani ya Sh. bilioni 350.36 mwaka 2019/20 hadi kufikia mali zenye thamani ya Sh. bilioni 423.99 mwaka 2022. Ukuaji huu ni sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 10.51 kwa mwaka," alisema Dk. Doriye.

Alifafanua kuwa mtaji wa NIC umeongezeka kwa asilimia 100.4 kutoka Sh. bilioni 72.16 mwaka 2019/20 hadi Sh. bilioni 217.07 mwaka wa 2021/22. Ukuaji huu wa mtaji ni sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 100.40 kwa mwaka.

Pia alisema uwekezaji katika hati fungani za Serikali kwa mwaka 2021/22 umefikia Sh. bilioni 105.64 ikilinganishwa na Sh. bilioni 51.58 mwaka 2019/20.

"Uwekezaji katika amana za benki mwaka 2021/22 umefikia Sh. bilioni 32.23 ukilinganishwa na Sh. bilioni 19.53 kilichokuwepo mwaka 2019/20...ongezeko hili ni sawa na wastani wa asilimia 32.54 kwa mwaka," alisema.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa kwa tasnia ya bima ni uelewa mdogo wa wananchi kujua faida na bidhaa za bima ili waweze kunufaika nazo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI
(RUWASA)

## TANGAZO LA MNADA

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, Serikali itauza kwa njia ya Mnada wa Hadhara Magari, Pikipiki, Mitambo na vifaa mbalimbali chakavu katika Mikoa ya , **Dar es Salaam, Mara, Rukwa, Dodoma na Simiyu katika vituo na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini.**

**1. MKOA WA DAR ES SALAAM**

| TAREHE | KITUO | AINA YA MALI ZITAKAZOUZWA |
|---|---|---|
| 28/09/2023 | UBUNGO | Mitsubishi - Pick Up |
| | | Rig Carrier |
| | | Isuzu - Lorry |
| | | Nissan UD - Truck |
| | | Isuzu - Truck |
| | | Volvo - RIG Carrier |
| | | Volvo - RIG Carrier |
| | | Volvo - RIG Carrier |
| | | Volvo - RIG Carrier |
| | | Volvo - RIG Carrier |
| | | Margus - RIG Carrier |
| | | Nissan UD |
| | | Nissan UD - Crane |
| | | Compressor |
| | | Pick Up - Screpper |

**2. MKOA WA DODOMA**

| TAREHE | KITUO | AINA YA MALI ZITAKAZOUZWA |
|---|---|---|
| 30/09/2023 | DODOMA | Isuzu Lorry |
| | | Toyota Coaster |
| | | Isuzu Tipper - Lorry |

**3. MKOA WA SIMIYU**

| TAREHE | KITUO | AINA YA MALI ZITAKAZOUZWA |
|---|---|---|
| 03/10/2023 | MEATU | Motorcycle |
| 03/10/2023 | MEATU | Motorcycle |
| 02/10/2023 | BARIADI | Motorcycle |

**4. MKOA WA MARA**

| TAREHE | KITUO | AINA YA MALI |
|---|---|---|
| 04/10/2023 | RORYA | Toyota Land Cruiser S/Wagon |
| 04/10/2023 | TARIME | Motorcycle |
| 05/10/2023 | TARIME | Motorcycle |
| 05/10/2023 | SERENGETI | Motorcycle |
| 05/10/2023 | SERENGETI | Motorcycle |
| 05/10/2023 | SERENGETI | Motorcycle |
| 04/10/2023 | RORYA | Motorcycle |
| 04/10/2023 | RORYA | Motorcycle |
| 05/10/2023 | BUNDA | Motorcycle |
| 05/10/2023 | BUNDA | Motorcycle |
| 05/10/2023 | BUNDA | Motorcycle |

**5. MKOA WA RUKWA**

| TAREHE | KITUO | AINA YA MALI ZITAKAZOUZWA |
|---|---|---|
| 09/10/2023 | NKASI | Toyota Land Cruiser S/Wagon |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa papohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya Chombo/Kifaa alichonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa Chombo/kifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
4. Ruhusa ya kuangalia vyombo itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada husika;
6. Mnada utaanza saa Nne (04:00) asubuhi katika kila kituo.

MKURUGENZI MKUU
RUWASA

217594802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa madaktari uzingatiwe kujiepusha ugonjwa selimundu

**TANZANIA** ni kati ya nchi zinazokabiliwa na tatizo la ongezeko la wagonjwa wa selimundu (sickle cell) na mikoa ya Kanda ya Ziwa ikitajwa kuwa na wagonjwa wengi.

Kuongezeka kwa ugonjwa huo nchini kunasababishwa na watu kutokuwa na utaratibu wa kupima afya zao na kujua hali zao kabla ya kuingia kwenye ndoa.

Kwa mujibu wa madaktari bingwa watu wanaoingia kwenye uamuzi wa kufunga ndoa ili kuwa mke na mume ni vema wakapima hali zao kujua kama wana vinasaba vya selimundu ili kuepuka kuzaa watoto wenye ugonjwa huo.

Tanzania inaelezwa kuwa ni nchi ya tano duniani kuwa na wagonjwa wengi wa selimundu na ndoa zenye watu wenye vinasaba vyenye ugonjwa huo zinachochea watoto kuzaliwa na tatizo hilo.

Kila mwaka nchini Tanzania watoto 14,000 huzaliwa na ugonjwa huo huku 10,000 kati yao huzaliwa mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mkoa wa Mwanza ukiwa na idadi kubwa.

Matibabu ya ugonjwa huo yanafanyika kwa kupandikiza uloto kutoka kwa ndugu wa karibu kwenda kwa mtoto mwenye tatizo.

Huduma hii huweza kugharimu Sh. milioni 30 hadi milioni 40, jambo ambalo ni gumu kwa Watanzania wenye maisha duni.

Kuepuka tatizo hilo ni lazima jamii ikubaliane kupima kabla ya ndoa ili kuwaepusha watoto na maumivu wanayopitia.

Kwa mwaka 2022 Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tabora Kitete, kulikuwa na jumla ya wagonjwa 386 waliolazwa wodi ya watoto kwa sababu ya changamoto za kiafya za ugonjwa huo na wengine 291 kuhudhuria kliniki ya selimundu na mwaka 2023 kuanzia Januari hadi Mei jumla ya wagonjwa 188 walilazwa na 133 walihudhuria kliniki.

Takwimu hizo zinaonesha kuwa hali hiyo siyo nzuri na inatakiwa vyombo vinavyohusika kutoa elimu kwa wananchi vifanye kazi hiyo ili kuwaepusha Watanzania na tatizo hilo kwa kuchukua tahadhari mapema.

Kwa mujibu wa wataalamu, inakadiriwa kuwa ni asilimia 20 ya Watanzania wanabeba vinasaba vya ugonjwa wa selimundu ambao unaongezeka mwaka hadi mwaka tatizo lililogunduliwa katika Hospitali ya Rufani Kitete kutokana na idadi kuongezeka kwa wagonjwa wanaofika kupata huduma.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto Mkoa wa Tabora, Dk. Amon Ryakitimbo, alisisitiza umuhimu wa jamii kabla ya kufunga ndoa kwenda hospitali kwa ajili ya kupima ugonjwa huo ili kujua afya zao na kuepusha kupata watoto wenye tatizo hilo.

Nia kubwa ya kupima ni kujua tatizo la ugonjwa huo kama ni mbebaji wa kinasaba kwa sababu kuna njia ya kujikinga na madhara yanayotokana na ugonjwa huo kwa kufuata kanuni na taratibu za kitabibu.

Kinachotakiwa ni jamii kuwa na uelewa wa tatizo la ugonjwa huo ambao humfanya mtoto anayezaliwa kupungukiwa damu mara kwa mara na hata ukuaji wake huwa tofauti na mtoto aliyezaliwa bila kuwa na vinasaba hivyo.

Watoto wengi hupoteza maisha kutokana na wazazi wao kutoelewa tatizo hilo na kufikiri labda wamerogwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Kila la heri la saba, epukeni ujanjaujanja

**KESHO** wanafunzi wa darasa la saba, wanaanza mtihani wa taifa wa kuhitimu elimu ya msingi, unaofanyika Jumatano na Alhamsi.

Wakati wakiwa katika maandalizi ya mtihani huo, ni vyema kuwakumbusha kwamba wasikubali kujihusisha na udanganyifu pia kudanganywa kwa sababu kunaweza kuwakwamisha kwenye safari hiyo ya kitaaluma

Ninakumbushia hilo, kwa sababu kila mwaka baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakifutiwa matokeo ya mtihani kutokana na kile kinachodaiwa kuwapo kwa udanganyifu katika mitihani hiyo.

Wakati baadhi yao wakifanya udanganyifu, wengine huambiwa na wazazi au walezi wao wasifanye vizuri mitihani hiyo, ili wafeli warudi nyumbani waolewe au wafanye majukumu mengine ya nyumbani.

Mitindo hiyo ni wazi kwamba haina manufaa kwa mwanafunzi zaidi ya kumharibia maendeleo yake kwenye elimu.Hivyo ninadhani ni vyema wakaachwa wafaulu kulingana na uwezo wao darasani.

Lakini pia wasielekezwe kufanya mitihani kwa kujikosesha ili hatimaye wasifaulu, kitendo ambacho, ninadhani kinakwamisha maendeleo ya mtoto wa kike na wa kiume katika elimu.

Wale wanaofanya udanganyifu katika mitihani na kufaulu, ni wazi hawawezi kuwa na msaada kwa taifa, kwani pamoja na kuonekana kuwa wamefaulu, lakini mbele ya safari watakwama.

Watakwama kwa sababu, hawakufaulu kwa akili zao, bali ni kutokana na kuonyeshwa majibu, hivyo inaweza kuwa vigumu kuwa na uelewa wa kutosha katika masomo ya ngazi ya juu.

Ikumbukwe kuwa njia hiyo ya kufanya mitihani, inafanikisha kutambua uwezo wa kila mwanafunzi kielimu, ili kadri wanavyoendelea na elimu ya juu, waweze kuwekwa katika makundi kulingana na kile wanachotamani kukifanya, ili hatimaye kuweza kupata wataalam wa baadaye.

Lakini, wanapofanyiwa mitihani au kuwapo kwa udanganyifu wa aina yoyote ya kumwezesha mwanafunzi afaulu, ninadhani hatua hiyo imekaa vibaya haiwezi kumsaidia mwanafunzi.

Ni vyema kuwa na wanafunzi waliofaulu kulingana na uwezo wao wa darasani, ambao baadae watakuwa na manufaa kwa taifa lao kupitia taaluma walizosomea, kwani kinyume cha hapo ni sawa na wasomi 'feki'.

Upande wa pili wa wazazi na walezi ambao huwa wanawaambia watoto wao wajikoseshe kwa kuweka majibu ambayo sio katika mitihani, ili wasifaulu, hao wanaharibu ndoto za watoto wao katika elimu.

Ninadani walimu wamewaandaa wanafunzi vizuri, hivyo waachwe wafanye mitihani kwa kuzingatia kanuni za mtihani ili matokeo yaonyeshe uwezo wao halisi kulingana na maarifa na ujuzi waliopata.

Wanafunzi wanaofanya mitihani wanapaswa waonekane wamepata elimu bora na sio bora elimu, ili waweze kumudu ushindani uliopo sasa duniani na kwenda sambamba na maendeleo ya haraka ya sayansi na teknolojia.

Mbinu za aina yoyote za kumsaidia mwanafunzi afaulu au afamye vibaya mitihani zitarudisha nyuma maendeleo ya elimu na juhudi za kuliweka taifa katika uwiano unaotakiwa katika elimu na mataifa mengine.

Ikumbukwe kwamba, mwanafunzi ambaye atakuwa amefaulu kwa ujanjaujanja na udanganyifu, lazima utendaji kazi wake utakuwa na walakini na upungufu mkubwa ikilinganishwa na aliyefaulu kihalali.

Vilevile, ikumbukwe kuwa mzazi au mlezi kumwelekeza mtoto wake kujikosesha majibu ya mtihani ni sawa na kuhujumu ndoto za mtoto ambazo amejiwekea katika elimu.

Ipo haja kuunga mkono juhudi za serikali za kutaka kila mtoto apate elimu, hasa baada ya kuamua kutoa elimu bure kuanzia ya msingi hadi kidato cha sita.

Iwapo lengo hilo litaachiwa lifanye kazi, ni wazi kila mtoto anaweza kutimiza ndoto yake katika elimu, na kuifanya nchi kupata wataalam wengi wa baadaye wa fani mbalimbali.

Hivyo, niwatakie kila la heri wanafunzi wote wanaojiandaa kufanya mtihani wa taifa wa kuhitimu elimu ya msingi. Mbinu zote chafu zisipewe nafas, wafanye mtihani bila kuingiliwa.

## HABARI KITAIFA

# TRC, WFP yazindua mabehewa kusafirisha mazao

**Na Faustine Feliciane**

WAKULIMA wa mboga na matunda katika mikoa ya Dodoma na Morogoro wamepata neema ya kusafirisha bidhaa zao Dar es Salaam baada ya Shirika la Reli Nchini (TRC) kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), kuzindua mabehewa maalumu yenye jokofu yatakayotumika kusafirishia mazao hayo.

Akizindua mabehewa hayo jana jijini Dar es Salaam, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, alisema yatatumika kutoa bidhaa hizo kutoka mikoa hiyo na kwenda moja kwa moja Dar es Salaam kwenye masoko.

Alisema wakulima wa mazao hayo kama watatumia vizuri usafiri wa reli kutoka katika mikoa hiyo utawaongezea ufanisi kwenye kilimo chao na kuwaongezea kipato.

"Nitoe maagizo kwa TRC ihakikishe huduma hii ya usafiri kutumia mabehewa iwe endelevu na kuweka gharama rafiki kwa wakulima, lengo ni kuwasaidia kusafirisha bidhaa zao kuja Dar es Salaam bila kuharibika na kumpunguzia hasara mkulima," alisema Profesa Mbarawa.

Aliitaka TRC kufanya utaratibu wa kuongeza mabehewa hayo kutoka matano ya sasa na kuwa mengi ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

Mkurugenzi na Mwakilishi Mkazi wa WFP, Sarah Gordon-Gibson, alisema kupatikana kwa mabehewa hayo kutatoa fursa kwa mikoa ya Dodoma na Morogoro wakulima kuwa na uhakika wa kusafirisha bidhaa zao bila kuogopa kuharibika njiani.

"WFP tunajivunia kufanikisha kupatikana kwa mabehewa haya, tutaendelea kushirikiana na TRC na serikali kwa ujumla kuweka mazingira mazuri kwa wakulima wa mboga kutoka mikoa ya mbali na Dar es Salaam," alisema Sarah.

Alisema mabehewa hayo matano yaliyozinduliwa jana yamegharimu zaidi ya Sh. milioni 800.

Kaimu Mkurugenzi wa TRC, Amina Lumuli, alisema Shirika hilo litatanua huduma hiyo na kufikia mikoa ya Kanda ya Ziwa na mingine yenye huduma ya usafiri wa reli wa shirika hilo.

"Kwa kuanzia tumeanza na mikoa hii miwili, lakini lengo ni kusambazwa huduma hii katika mikoa yote inayozalisha mazao ya mboga na matunda.

Alisema mabehewa hayo yana uwezo wa kubeba zaidi ya tani 200 ya mazao ya mboga na matunda.

Mwakilishi wa wadau wa mazao hayo, Ally Mbuguyo, alisema kuwapo kwa mabehewa hayo ni neema kwao kama wafanyabiashara na yataongeza tija kwenye biashara zao.

"Lakini pamoja na kupatikana mabehewa haya na kuanza kutoa huduma, bado mahitaji ni makubwa sana, mabehewa haya matano hayawezi kukidhi, tunaomba TRC na WFP muangalie uwezekano wa kuyaongeza pamoja na wigo wa usafiri huo kufika katika mikoa mingine inayozalisha mazao haya," alisema Mbuguyo.



Shughuli ya utoaji tope lililoziba daraja la Jangwani, pamoja na kupanua mtaro wa bonde la Mto Msimbazi ikiendelea, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mgombea wa CCM aahidi neema Jimbo la Mbarali

**Na Halfani Chusi**

MGOMBEA Ubunge Jimbo la Mbarali, Bahati Ndingo ameahidi kuwasaidia wakulima kupata kwa wakati pembejeo za kilimo ikiwamo mbolea na viuatilifu ili kuepuka gharama ya kuvifuata mbali kama ilivyokuwa awali.

Aliahidi kusaidiana na serikali kushauri njia nzuri ya kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Ruaha na wanakijiji kwa kuwa yeye ni mzoefu na mwenyeji wa eneo hilo.

Bahati, alitoa ahadi hiyo jana kwa njia ya simu alipoulizwa na mwandishi wa habari hizi kuhusu msimamo wake iwapo atapata ridhaa ya kuongoza jimbo hilo.



Alisema, mwaka jana wakati wa msimu wa kilimo, waliopewa tenda ya kusambaza mbolea ya ruzuku walikuwa wachache na watu wa Mbarali walikuwa wanalazimika kuifuata mbali jambo lililokuwa linawaongezea gharama.

"Wakulima walikuwa wanaenda mbali walikuwa wanafika mpaka Makambako na maeneo mengine, wanatumia gharama kubwa, kikubwa jibu hapa ni kuiomba serikali kupanua utolewaji wa huduma hizo kwa kuongeza vituo ili kuwapunguzia gharama wakulima.

"Rais Samia amewekeza fedha nyingi ili kumpunguzia gharama mkulima, kwahiyo, kunapaswa kuwe na vituo vingi maeneo yaliyo karibu na wakulima, kwa sababu inapokuwa haipatikani jirani na wakulima wanapotumia gharama inakuwa hakuna maana ya ruzuku tena," alisema.

Alisema, wakati anapita kwenye maeneo hayo kwaajili ya kuomba kura alikutana na kilio cha wananchi kuhusu kero ya maji, barabara, shule na vituo vya afya jambo aliahidi kuanza nalo.

"Kipekee ninampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuboresha miradi mbalimbali kwenye eneo hili, fedha nyingi zimetumika. Kajenga na kuongeza vituo vya afya, vipo tunaongelea zaidi ya bilioni kumi zimetumika.

"Tuna mradi wa maji kule Ruduga Mawindi zaidi ya bilioni tano zimetumika, kata ya mapogoro bilioni 44 kwaajili ya miradi ya umwagiliaji, mradi wa umwagiliaji madibilia umegharimu zaidi ya bilioni nane, kwenye elimu ya sekondari zaidi ya bilioni tatu zimetumika kuimarisha miundombinu ya shule na ujenzi wa josho katika kila kata.

Alipoulizwa kuhusu wakazi wengi eneo hilo kukosa elimu, alisema bonde hilo lina ng'ombe wengi na wafugaji bado wanashikilia mila za kizamani kuwanyima watoto haki ya kusoma na kuwaacha wakichunga.

"Tutaendelea kuhamisha na kutoa elimu kwa wakazi wa huku mbarali kwa kuwa serikali imeweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa elimu bure, wengi bado uelewa ni mdogo, watoto wanapelekwa kuchunga na wengine wanajifelisha makusudi kupitia amri za wazazi," alisema.

Mgombea huyo anawania nafasi hiyo baada ya aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Francis Mtega, kufariki kwa ajali na kufanyika uchaguzi mdogo kwa ajili ya kupata mrithi.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# IPTL, TANESCO kukutana tena kortini

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imetoa wito kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kufika mahakamani kesho kwa ajili ya kesi kati yake na Kampuni ya Kufua Umeme ya IPTL.

Wito huo ulitolewa jana na Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ambapo mdai katika shauri hilo ni IPTL na mdaiwa TANESCO.

Shauri hilo linatarajiwa kusikilizwa mbele ya Jaji Fatma Maghimbi, mdaiwa anatakiwa kufika bila kukosa akiwa na nyaraka anazotarajia kutumia katika shauri hilo.

IPTL kwa mujibu wa kumbukumbu zake za fedha hivi karibuni, inaidai TANESCO zaidi ya Dola za Marekani milioni 700 ambazo hadi sasa haijalipwa.

Kuna kesi nyingine namba 112 ya 2009 katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kuhusu madai ya Dola za Marekani milioni 138.

IPTL inadai kuwa Septemba 15, 2010, Benki ya Standard Charterd Hong Kong (SCBHK) ilianzisha kesi za Usuluhishi Na. ARB/10/20 katika Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro (ICSID) kutafuta tuzo kutoka TANESCO kutokana na uamuzi wa mahakama.

"Cha kufurahisha mashauri haya ya usuluhishi yalianzishwa kinyume cha sheria na SCBHK wakati IPTL iliwekwa chini ya muda kufutwa kutokana na uamuzi wa Mahakama Kuu, amri iliyotolewa Desemba 16, 2008.

"Amri hiyo ilikuwa haihusiani na Mkataba wa Ununuzi wa Nguvu (PPA) ambayo TANESCO ilikuwa imeingia na IPTL," inadai IPTL.

Inadaiwa kuwa Agosti 26, 2014, Mahakama Kuu Masjala Kuu Dar es Salaam katika maombi Na. 174 ya mwaka 2014, kati ya IPTL, PAP dhidi ya SCBHK na TANESCO, ilitoa amri ya zuio, kuzuia SCBHK na mawakala wake pamoja na mambo mengine kuiondoa IPTL au kuingilia kwa namna yoyote.

Wakati usimamizi wa mtambo wa kufua umeme wa IPTL ulio Tegeta ukiendelea, kuna kesi ya msingi katika kesi ya madai namba 60 ya 2014, ilianzishwa na IPTL na PAP katika Mahakama Kuu Dar es Salaam Masjala ya Wilaya ambako IPTL na PAP, pamoja na mambo mengine, wanataka tamko kwamba uamuzi uliotolewa na ICSID katika kesi Na. ARB/10/20 ni batili.

Inadaiwa ulipatikana kwa ulaghai na IPTL pia inadai Dola za Marekani bilioni 3.2 ambayo ni hasara iliyosababishwa na SCBHK kwa uvunjaji wa mkataba wa nguvu kati yake na TANESCO.

Kituo hicho cha kimataifa chenye makao yake Washington kilitoa amri hiyo katika kesi iliyoanza mwaka 2001 kuhusu ununuzi, makubaliano ya Mei 1995 kati ya TANESCO na Independent Power Tanzania Ltd, ambao haki zao baadaye zikachukuliwa na Standard Chartered miaka minne iliyopita.

Mkataba huo uliitaka IPTL kuipatia TANESCO 100MW kabla ya kampuni kufutwa Desemba 2008 kufuatia migogoro ya umiliki kati ya wanahisa wake.

TANESCO katika rufani yake, ilishikilia kuwa ililipa IPTL wakati Standard Chartered alidai kuwa alipaswa kulipwa badala yake.

Mwaka 2016, ICSID iliamuru TANESCO kuilipa benki ya SCBHK Dola za Marekani milioni 148.4.

Fedha hizo ni madai ya malipo ya umeme baina ya TANESCO na Kampuni ya IPTL iliyopewa zabuni ya kufua umeme wa dharura kuanzia Mei 26, 1995 huku ikidaiwa na benki hiyo.

IPTL ilikuwa ikidaiwa na benki hiyo ya Hong Kong kutokana na mkopo iliyochukua kutekeleza mkataba kati yake na TANESCO.

Novemba 2017, TANESCO iliwasilisha gharama zake, nyaraka zinaonesha shirika tayari limelipa gharama za mahakama.



Gavana wa Kanda wa Rotary, Ssemwanga Franciso (aliyevaa suti) na Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam, Nikki Aggarwal, wakiserebuka pamoja wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtakuja iliyopo Kunduchi Mtongani katika hafla ya kukabidhi madawati 100 yaliyotolewa na klabu hiyo. Hadi sasa klabu hiyo imetoa madawati takribani 2,500 yenye thamani ya Sh. milioni 400 kwa shule mbalimbali za msingi mkoani Dar es Salaam. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Utouh: Tusipochukua hatua, dunia haitakuwa salama kwa kizazi kijacho

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, ameshauri hatua madhubuti zichukuliwe kitaifa na kimataifa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Amesema hatua stahiki zisipochukuliwa kukabiliana na baa hilo, anaona hatari ya dunia kutokuwa mahali salama kwa kuishi kwa kizazi kijacho.

"Tayari tumeshuhudia mabadiliko katika barafu ya Mlima wetu wa Kilimanjaro. Tumeona pia mifugo kule Longido na Kenya ikifa. Mabadiliko ya tabianchi yamemwathiri kila mtu duniani," alisema jana.

Utouh, aliyewahi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alikuwa anazungumza na waandishi wa habari ofisini kwake wilayani Kinondoni, Dar es Salaam kuhusu Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC) utakaofanyika Septemba 28 na 29 mwaka huu jijini Arusha, ukiandaliwa na Taasisi ya WAJIBU.

Ni mkutano wa tatu tangu taasisi hiyo ilipoanza kuandaa mikutano ya aina hiyo mwaka 2021, safari hii ukibeba maudhui ya Kuimarisha Uwajibikaji kwa Mabadiliko ya Tabianchi, ukiwa na mada mbalimbali ikiwamo ya kumulika vihatarishi vya kifedha katika mabadiliko ya tabianchi.

Utouh alisema wanatarajia kuwa na washiriki 300 katika mkutano huo wanaotoka taasisi za serikali, wadau wa maendeleo, wanadiplomasia, wanaazaki, wabobezi wa masuala ya uwazi na uwajibikaji, wabobezi wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi, wanataaluma mbalimbali na waandishi wa habari kutoka ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

"Tunategemea mkutano huo kuwa na watoa mada wa kimataifa ili kuleta ladha ya kimataifa kwa kupata uzoefu wao katika nchi sita ambazo ni mwenyeji Tanzania, Afrika Kusini, Kenya, Zimbabwe, Nigeria na Zambia," alisema.

Utouh alisema wahiriki watapata fursa kubadilishana ujuzi na uzoefu, usimamizi mzuri zaidi wa fedha zinazohusika na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kutambua vihatarishi vilivyopo na namna ya kushughulikiwa na kupanga wakati wa ushiriki wa pamoja kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi hayana mipaka.

Mkurugenzi huyo alisema maelezo zaidi ya namna ya kushiriki katika mkutano huo yanapatikana katika tovuti ya taasisi hiyo, yakijumuisha kuchangia Sh. 25,000 kwa wenyeji na Dola za Marekani 15 kwa wageni.

## Chanzo cha maji hatarini kutoweka

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

SHUGHULI za kibinadamu katika chanzo cha maji Bwawa la Ning'hwa lililoko Chibe, Manispaa ya Shinyanga, kiko hatarini kukauka kutokana na shughuli za binadamu.

Bwawa hilo hutumika kama chanzo mbadala cha kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa Shinyanga, pale chanzo kikuu cha maji ya Ziwa Victoria kinapopata hitilafu.

Kabla ya kuunganishiwa maji toka Ziwa Victoria, wakazi wa Mji wa Shinyanga walitumia maji ya Bwawa la Ning'hwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Yusuph Katopola, baada ya kutembelea bwawa hilo juzi, alisema jitihada zinahitajika ili kukinusuru chanzo hicho kisitoweke kwa kuwa bado ni msaada mkubwa katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

Alisema wananchi wanapaswa kupewa elimu ya kutosha ili waache kufanya shughuli za kibinadamu katika bwawa hilo, ikiwamo uvuvi, kuchunga mifugo na kilimo ambacho kimekuwa kikisababisha udongo kuingia katika bwawa na kuanza kupunguza kina na kutoweka polepole.

"Hali ikiendelea kuwa mbaya zaidi, bwawa hili litakauka kabisa. Itabidi tuzime mitambo yetu na kuacha kulitumia kuzalisha maji na tuendelee kutumia chanzo kimoja cha Ziwa Victoria kwa kununua maji kutoka kwa wenzetu KASHWASA. Itasababisha gharama za maji kuwa juu," alisema.

Katopola aliwataka wananchi wanaolizunguka bwawa hilo waache mara moja kufanya shughuli za kibinadamu, ili kukinusuru chanzo hicho cha maji na kuendelea kunufaika nacho.

Msimamizi wa Bwawa hilo kutoka Ofisi Ndogo za Bonde la Kati, Ninje Kashindye, alisema kwa sasa kina cha maji kimepungua na kubaki mita tano kulinganishwa na uwezo wa bwawa hilo, ambalo likijaa, lina ujazo wa mita milioni 10.6.

Alisema wamekuwa wakijitahidi kuzuia wananchi kufanya shughuli za kibinadamu kwa kuwapatia elimu kuhusu madhara ya shughuli hizo katika bwawa hilo, lakini wanakaidi na wakati mwingine wakiwafuata huwatisha hata kuwapiga.





# Wajenga shule kuwanusuru watoto wao mwendo mrefu

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WAKAZI wa Losiai, Luhondo na Mafisa katika kijiji cha Makelele, Kata ya Pagwi, Wilaya ya Kilindi, wamejenga shule kwa kujitolea ili kulinda maisha ya watoto wao wanaolazimika kuvuka mto kwenda shule umbali wa kilometa saba.

Wakizungumza kwenye harambee ya ujenzi wa shule hiyo inayojengwa katika kitongoji cha Losiai, wananchi hao walidai kuwa licha ya umbali, lakini watoto wao wanakabiliwa na athari mbalimbali ikiwamo mito mikubwa wanayovuka wakienda shule pamoja na vichaka wanamopita.

Walisema kutokana na hali hiyo wameamua kwa hiari yao kujenga shule hiyo pia wataomba kupata usajili ili kuwa shule kamili baada ya kukamilika na kuiomba serikali kuunga mkono.

Elias Makanyaga mkazi wa kitongoji cha Mafisa, alisema kiwango cha elimu kwa watoto wao kinashuka wakati wa mvua kutokana na wanafunzi kushindwa kwenda shule kutokana na mito kujaa maji.

Wilfred Majele, mkazi wa kitongoji cha Luhondo, alisema wameamua kujenga shule hiyo ili kuokoa maisha ya watoto wao kwa kuwa wakati wa mvua hawana amani hususani watoto wao wanapokuwa shuleni kukwama kurudi nyumbani.

Mwajabu Omari, mkazi wa kitongoji cha Luhondo, alisema kero imewasumbua kwa miaka mingi, kukamilika kwa shule hiyo kutajenga imani ya usalama wa wanafunzi hao.

Joyce Chijo, aliushukuru uongozi wa Serikali ya Kijiji cha Makelele kwa kutoa eneo linalojengwa shule hiyo pamoja na kumpongeza Ofisa Tarafa wa Kwekivu, Michael John kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara wa changamoto zinazowakabili wakazi wa tarafa hiyo na kutoa ushauri kwa wananchi wenzake kuunga mkono juhudi hizo.

John alisema lengo la serijali ni kuhakikisha kila mwanafunzi anapata elimu bila ya kutembea umbali mrefu na kwamba changamoto hiyo ni miongoni mwa mambo yaliyokuwa yakiwasumbua wakazi wa vitongoji hivyo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Makelele, Frank Meshack, alisema mkutano mkuu wa kijiji uliridhia eneo la ekari 60 kujengwa shule hiyo kutokana na changamoto ya watoto kutembea umbali wa kilometa saba hadi kijiji mama cha Makelele.

# ‘Kuna umuhimu kuimarisha mifumo ya usimamizi afya’

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amesema kuendelea kulinda afya na usalama wa wafanyakazi, serikali ina wajibu mkubwa wa kushirikiana na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa afya na usalama ili nguvu kazi inayotegemewa kwa maendeleo ya nchi ilindwe.

Prof. Ndalichako aliyasema hayo jana mkoani hapa, wakati akifungua mafunzo na ziara ya wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kuhusu masuala ya usimamizi wa afya na usalama mahala pa kazi.

Alisema kuwa masuala ya afya na usalama, ni mtambuka na yanagusa sekta zote za uchumi, lazima serikali kuimarisha mifumo ya afya kwa nguvu kazi.

“Tutambue kuwa ulimwengu wa kazi unakabiliwa na vihatarishi vingi vitokanavyo na ukuaji wa uchumi, mabadiliko ya teknolojia na ushindani wa kibiashara na yote haya, yanahitaji mbinu mpya au mbadala wa kubaini na kudhibiti athari ya vihatarishi hivyo,” alisema Prof. Ndalichako.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, katika kulinda nguvu kazi ya taifa pamoja na uwekezaji uliopo nchini, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ina jukumu la kukagua maeneo ya kazi na kufanya uchunguzi wa afya za wafanyakazi, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya namna ya kukabiliana na kudhibiti vihatarishi hivyo.

Alisema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji na waajiri ili waweze kuleta ajira na kuchangia kukuza pato la taifa, hivi karibuni serikali kupitia OSHA imeondoa tozo 13 zilizopunguza kero na gharama.

“Pia tumepunguza tozo ya umeme, katika vituo vya mafuta vijijini, kutoka 650,000 hadi kufikia 150,000, tozo hizi zilizofutwa na OSHA zimeleta unafuu kwa wafanyabiashara na wawekezaji nchini, kwa kuwapunguzia gharama za uendeshaji, kwa kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 35 endapo zingeendelea kutozwa,” alisema.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema kwa takwimu za Shirika la Afya Duniani, inaonyesha kuwa kila mwaka, watu 2,300,000 wanakufa kutokana na ajali mahala pa kazi na nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Julai mwaka 2020/21 ajali zilizoripotiwa zilikuwa 1,889, kati ya hizo vifo vilikuwa 7,500.

“Kutokana na ajali hizi mahala pa kazi gharama za fidia zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 13.19 kwa kipindi kilichoishia Juni mwaka 2021, hadi kufikia Sh. bilioni 17.93 kwa kipindi kilichoishia Juni mwaka 2023, hivyo kuna haja ya kuhakikisha gharama hizi na madhila vinapungua, kwa kila mwajiri kusimika mifumo ya afya na usalama mahala pa kazi,” alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya bajeti Daniel Sillo, alisema kuwa wanashukuru kwa mafunzo hayo yatakayowawezesha kupata uelewa zaidi na kuelimisha jamii umuhimu wa suala hilo, kwa kuwa wanapokuwa na jamii au wafanyakazi wenye afya, tija inaongezeka.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema kuwa vihatarishi ni vingi sehemu za kazi, mafunzo hayo yatawaonyesha moja kwa moja vihatarishi hivyo ikiwa ni pamoja na mifumo ya kudhibiti.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kijiji cha Mamboleo wilayani Muheza, mkoani Tanga, Ramadhani Kazuvi, akizungumza na wanafunzi wa darasa la saba shuleni hapo jana katika maandalizi ya Mtihani wa Taifa ambao utafanyika Jumatano Septemba 13 na 14 mwaka huu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waliofuzu mafunzo JKT watakiwa kukiishi kiapo

**Na Hamida Kamchalla,** MKINGA

VIJANA waliomaliza mafunzo ya awali ya kijeshi kwa mujibu wa sheria, kikosi 838 Maramba JKT, operesheni miaka 60 ya jeshi hilo wametakiwa kwenda kukiishi kiapo walichoapa kwa kulitumikia taifa lao kiuzalendo.

Serikali inatumia fedha nyingi kuyaendeleza ili kupata vijana ambao watakuwa wazalendo kwa taifa na inawapasa kuyatumia vema mafunzo hayo kuwa mabalozi wazuri kwa vijana wenzao na hata wazazi ambao wanawazuia watoto wao kujiunga.

Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Kanali Maulidi Surumbu, alitoa wito huo wakati akifunga mafunzo hayo na kusisitiza vijana mafunzo ya stadi za kazi waliyopatiwa yawasaidie kuwaletea maendeleo yao binafsi.

“Mzingatie mafunzo mliyopata kwa muda wote mliokuwa hapa ili yaweze kuwa chachu ya maendeleo yenu binafsi pamoja na taifa, lakini mtambue kwamba taifa lina matarajio makubwa sana kwenu na ndio maana tunatumia fedha nyingi kuhakikisha mnapata mafunzo haya,” alisema.

“Taifa likiwa na vijana wenye nguvu na moyo wa kuipenda nchi yao hata maendeleo ya uchumi vinaimarika kwa kuwa vijana wenye uzalendo hulijenga taifa lao kwa moyo mmoja,” alisema Kanali Surumbu.

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Jokate Mwegelo, aliwaasa vijana hao baada ya kuhitimu mafunzo jukumu lao ni kuilinda, kuitetea na kuitumikia nchi yao kwa jinsi itakavyotakiwa.

“Ni matarajio yangu kwamba vijana hawa wameiva vizuri na wakitoka hapa watakwenda kuwa mabalozi wazuri kule majumbani kwao kwa kile walichojifunza, lakini na kwa nchi yetu pia, mimi nimependa zile stadi za kazi kwa vijana hawa.

“Sasa hivi stadi za vijana wengi ni kushika simu na kuchati, lakini unapokuwa na kazi kama hizi, utaweza kushika jembe na kulima bustani ya mboga na kujipatia kipato, kwa hiyo rai yangu kwenu vijana wenzangu, mna kazi kubwa ya kuisemea nchi yetu,” alisisitiza Mwegelo.


Mkuu wa Kikosi 838 Maramba JKT, Kanali Ashraf Hassan, alisema vijana hao walianza mafunzo rasmi Juni 19, mwaka huu na walifanya ndani ya majuma 12 mfululizo na walijifunza mambo mbalimbali ikiwa ni maelekezo kutoka makao makuu ya jeshi hilo.

Aidha, walisema wana furaha kupata mafunzo hayo ambayo yamewawezesha kujitambua na kujua nini maana ya uzalendo na kuwa timamu kwa kufuzu mafunzo ya awali ya kijeshi kwa kujifunza mambo mengi ambayo awali hawakuyafahamu.

“Tunamshukuru Mungu kwa kuhitimisha mafunzo haya ambayo yametujenga kiakili na kimwili pia, mimi nilikuwa nikisikia uzalendo tu, lakini sikujua hasa maana halisi, sasa naondoka hapa nikiwa timamu, naahidi kwamba kiapo nilichokula kitaishi ndani yangu na niko tayari kuitumikia nchi yangu kwa vyovyote nitakachoelekezwa,” alisema, Amani Omari kutoka Gairo.

“Tumejifunza kitu kikubwa sana katika maisha ambacho ni nidhamu, hapa tumekutana vijana wengi kutoka mikoa mbamimbali na kila mmoja ana tabia yake, lakini kupitia mafunzo haya watu wamenyooka, JKT sio linajenga taifa bali pia linatujenga sisi vijana kuwa wepesi wa kutekeleza maagizo,” alisema.

“Tumejifunza uzalishaji mali na tumeelewa vema, tukitoka hapa naamini kama vijana kuna watakaoendelea vyuoni, bado tuna uwezo wa kujiajiri katika kilimo na ufugaji na tukajiongezea kipato, tunaishukuru serikali yetu kwa kutulea na kutupatia mafunzo haya,” alisema Christina Humba.





# MUWASA yaagizwa kupeleka huduma jeshini

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, mkoani Mara, Daniel Komote, ameagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) kusambaza maji katika taasisi za serikali ikiwamo Shule ya Sekondari Tarime na kambi ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) huko Nyandoto.

Alitoa maagizo hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wiki iliyopita kilichoandaliwa kwa lengo la kujadili na kupitisha utekelezaji wa miradi.

Komote pia alitumia fursa hiyo kupongeza MUWASA Kanda ya Tarime kwa kuwapatia gari na vitendea kazi vingine kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kazi za kila siku katika halmashauri hiyo.

Meneja wa MUWASA Wilaya ya Tarime, Buriton Kajigili, alipokea maelekezo hayo na kuahidi kutembelea shule hiyo ili kuona kinachohitajika ili kufanya ununuzi wa vifaa, pia watafika katika kambi ya jeshi kuangalia namna ya kutatua changamoto ya kupata huduma ya maji.

**Alitoa maagizo hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wiki iliyopita kilichoandaliwa kwa lengo la kujadili na kupitisha utekelezaji wa miradi.**

Kajigili alisema ujenzi wa mradi mkubwa wa Rorya-Tarime-Sirari ambao chanzo chake ni Ziwa Victoria, ukikamilika utakuwa suluhisho kwa wakazi wa maeneo hayo.

Alisema katika Kanda ya Tarime wameweka mipango ya uboreshaji huduma ya maji katika makundi matatu ya mpango wa muda mfupi, wa kati na mrefu ili kukabiliana na kero ya maji katika Mji wa Tarime na viunga vyake.

"Mpango wa muda mfupi tutaongeza mtandao wa usambazaji wa maji katika baadhi ya maeneo ya mji Km 21 kwa Sh. milioni 140 ambazo tayari zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Kwa mpango wa kati, tutaboresha ubora wa maji kupitia chanzo cha chemichem ya Nyanduruma, usanifu wa kujenga mfumo wa kuchuja maji umekamilika. Kinachosubiriwa ni kupata kibali cha kujengwa," alisema.




Diwani wa Kata ya Kipunguni jijini Dar es Salaam, Stephen Mushi, akimkabidhi mfuko wa unga wa lishe ulioongezewa virutubishi, Mwenyekiti wa Kikundi cha Glory, Jovina Bankobeza, baada ya kuzindua mashine inayozalisha unga huo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPA yasaidia kukabili uhaba wa vifaa vya kujifungulia Bukumbi

**Na Neema Emmanuel,** SENGEREMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari (TPA), imeanza kutekeleza majukumu mbalimbali ya kijamii katika maadhimisho ya Wiki ya Bandari nchini kwa kutoa msaada wa vifaa vya kujifungulia vyenye thamani ya Sh. milioni 10 katika Kituo cha Afya Bukumbi kilichoko wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo juzi, Kaimu Meneja wa Bandari za Ziwa Victoria, Francisco Mwanga, alitaja vitu walivyotoa kuwa ni pamoja na vitanda viwili, kompyuta mbili na mashuka 123.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa kuhusu adha zinazowakabili katika kituo hicho zikijumuisha upungufu wa vifaa tiba katika kitengo cha mifupa, TPA ilikitaka kuwasilisha maombi.

Baadhi ya wajawazito katika kituo hicho waliiomba serikali na mashirika binafsi kuendelea kuona uhitaji wa kituo hicho ili kuondoa adha ya baadhi yao kujifungulia sakafuni kutokana na uhaba wa vitanda ulioko kituoni huko.

Kaimu Mganga Mkuu wa Kituo hicho, Pius Fred, alisema kuwa hatua za wadau kuona kero zinazokikabili kituo hicho hususani katika kitengo cha mama na mtoto inatoa faraja kwa watumishi na kuwapa fursa ya kufanya kazi katika mazingira rafiki.

Alieleza kuwa kompyuta walizopatiwa zitasaidia katika utunzaji kumbukumbu na kurahisisha huduma za kimfumo zinazopunguza foleni kwa wagonjwa kutokana na kituo kujikita zaidi katika huduma za kimfumo, badala ya kutumia karatasi ambazo husababisha pia uchafuzi wa mazingira.

# Mkulima alia na ukame, aomba msaada wizarani

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKULIMA wa Kijiji cha Lyagiti, Kata ya Lyabukande, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Shauri Mbelele, ameomba kuwezeshwa kuchimba mabwawa ya maji ili kuendesha kilimo chake.

Akizungumza na Nipashe kijijini huko jana, Mbelele alisema kazi yake kubwa ni kilimo, hivyo anaomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kumwezesha kwa kumchimbia mabwawa ya umwagiliaji ili aendeshe kilimo chenye tija.

Alibainisha kuwa kwa sasa ana shamba lenye ukubwa wa ekari 40 za mahindi yaliyo katika hatua ya kukomaa, lakini yameanza kukauka kutokana na kukosa mvua ya kutosha.

Mkulima huyo aliomba Wizara ya Kilimo kupitia wataalamu wake kutembelea kijiji hicho kujionea kilimo chake kilivyoathirika kutokana na ukame baada ya mabwawa aliyochimba kukauka.

Akisema kuchimbwa kitaalamu kwa mabwawa hayo kutakuwa msaada mkubwa kwa wanakijiji wote na kutoa fursa ya kuendesha kilimo pasi na kutegemea mvua.

Mkazi wa Kijiji hicho, Haruna Misamitana, alisema ni miongoni mwa vijana wengi waliohitimu masomo yao vyuoni, lakini hawana ajira rasmi, hivyo wakaamua kujikita katika kilimo.

Aliomba serikali kwa kushirikiana na asasi zinazotoa elimu ya kilimo kwa vijana, wasaidie kwa kuwachimbia kitalaamu mabwawa ya maji yatakayokuwa yanatunza maji ili walime kwa tija.

Ofisa Kilimo Manispaa ya Kahama, Richard Hegera, alisema wamekuwa wakitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo na kuwagawia vijana bure.

Masharti ni wanufaika kuwa na uwezo wa kulima walau ekari tano na mazao wanayopata ni mali yao na si ya halmashauri.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kutaka kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kuondoa wimbi la vijana wanaoshinda mitaani wakicheza michezo ya kubahatisha.

Ofisa huyo alisema wamekuwa wanawafikia mashambani na kuwashauri namna ya kulima kisasa na kuyatumia mabwawa yaliyoko katika kilimo cha umwagiliaji.

Hegera alisema kuwa kati ya kata 20 zilizoko Manispaa ya Kahama, ni kata 11 pekee za pembezoni ambazo wananchi wanajihusisha na kilimo cha chakula na biashara.

Alisema wamewawezesha maofisa ugani vyombo vya usafiri ili wawafikie wakulima na kuwashauri kulima kisasa kulingana na jiografia ya ardhi ya kila mkulima.




Ukurasa 12

Vijana wakizibaini tamu, chungu za mitandao ya kijamii watafanikiwa



Ukurasa 13

Ufugaji unavyowatoa vijana baada VETA kuwaanzishia program 'spesho'



Ukurasa 14

Maisha mapya kwenye mwezi ni dhahiri baada ya kuthibitika kuwa maji yapo


Nipashe

TESA

Jumanne Septemba 12, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

MWIBA NDOA UTOTONI

# Kutumia mabibi harusi feki mbinu inayobuniwa kukwepa rungu la dola

KATA ya Masengwa wilayani Shinyanga ni maarufu si kwa kilimo au maisha bora kwa wanavijiji laa, ila inatikisa anga kwa kukatisha masomo mabinti na kuwaozesha utotoni pia wakiwatumia mabiharusi feki kuficha ukweli.

Mchungaji wa Kanisa la Kipetentekoste PAG Shinyanga, Edward Salamba, akizungumzia vita ya kutokomeza ndoa kwa wasichana wadogo, anaiamsha serikali kwamba katika kudhibiti ndoa hizo za utotoni, wanapaswa kuwa makini sababu jamii imekuwa na mbinu nyingi ikiwamo kuweka mabibi harusi feki ambao wana zaidi ya miaka 18.

Mabinti hao wakubwa wanaweza kuoneshwa kuwa ndiyo wanaoolewa lakini kwa siri kuna bibi harusi halisi mtoto mdogo ambaye amefichwa kuhakikisha kuwa mpango huo haugunduliki.

Mchungaji anaitaka jamii kuzingatia maandiko matakatifu na sheria za nchi kuwalinda watoto wa kike kwani wanastahili kupendwa na kulindwa, hivyo iache kuwaozesha ndoa za utotoni na kutumia mbinu za kuficha ukweli ambazo hazisaidii taifa wala familia na wahusika wenyewe.

Lakini pamoja na bibi harusi feki, pia kuna kuwapeleka mabinti kushiriki kwenye ndoa za kimila maarufu 'bukwilima'.

Ndoa hizo ni mpango wa kufanikisha nia ya wasichana hao kushirikiana kingono na wanaume ambao humsindikiza bwana harusi lengo likiwa ni kuongeza ushawishi kwa wasindikizaji hao kuwaoa.



Ndoa ya binti wa miaka 15 iliyofungwa Malawi. **PICHA: MTANDAO**

Itakumbukwa kuwa takwimu za utafiti wa idadi ya watu na afya (TDHS) za mwaka 2015/2016, zinaeleza kuwa mwanamke mmoja kati ya watatu nchini huolewa kabla ya miaka 18, kadhalika utafiti huo unaonyesha kuwapo na ongezeko la asilimia 5 kwenye ndoa za wasichana walio katika rika balehe ambao ni umri kati ya miaka 15 hadi 19, ukilinganishwa na utafiti wa 2010.

Ofisa Mtendaji wa Masengwa, Hussein Majaliwa, akizungumza na Nipashe, anasema mikakati ambayo wamejiwekea katika kupambana na ndoa za utotoni, ni kutunga sheria ndogo kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji hadi kata zitakazopiga marufuku ndoa yoyote kufungwa kijijini bila ya kupata kibali kutoka serikali za mitaa.

Anasema wamefanya hivyo sababu walikuwa wamejisahau kuwalinda mabinti wadogo waliopo nyumbani ambao hawasomi na wengine waliomaliza darasa la saba lakini hawakuendelea na masomo ambapo wazazi huwaozesha ili kupata mifugo.

Majaliwa anasema baada ya kuligundua tatizo hilo wametunga sheria ndogondogo ambayo licha ya kuwalinda wanafunzi waliopo shuleni pia itawalinda mabinti majumbani wasiozeshwe utotoni bali wasubiri hadi watimize miaka 18.

"Tumefanya hivi ili kumaliza tatizo hili la ndoa za utotoni sababu baadhi ya wazazi hushawishi watoto wao wafanye vibaya mitihani ya darasa la saba ili wapate mwanya wa kuwaozesha kwa madai hawasomi shule kwa tamaa ya kupata mifugo,"anaongeza Majaliwa.

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Masengwa, Oliva Mayanza, anasema tangu kuanza kutumika kwa sheria hizo tatizo la ndoa za utotoni limepungua si kama miaka ya nyuma.

Anasema jamii nayo imeelimika na kutoa taarifa pale wanapoona mtoto akitishiwa kuozwa, na kwamba mwaka huu wamepokea taarifa ya ndoa ya mtoto na kuidhibiti na mwanafunzi kuendelea na masomo.

Aisha Omary, Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilayani Shinyanga, anasema ndoa za utotoni ni kikwazo kikubwa kwa maisha ya watoto wengi wa kike katika maeneo ya vijijini.

Anasema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wamekuwa wakipambana kutokomeza ndoa hizo, kwa kutoa elimu pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wazazi ambao huendekeza tamaduni za kuozesha watoto, na wamefanikiwa kuzipunguza.

"Ndoa za utotoni wilayani Shinyanga zimepungua, takwimu za mwaka jana zinaonyesha kupangwa kufungwa ndoa tatu ambazo tulikuwa na taarifa nazo na tulizitibua, lakini miaka ya nyuma zilikuwa zikifungwa hadi 10 kwa mwaka, na chanzo cha ndoa hizi ni mila na desturi kandamizi," anasema Aisha.

Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Kata ya Masengwa, Joyce Richard, anasema sheria ndogondogo na elimu ya madhara ya kuozesha ndoa za utotoni, imesaidia kupunguza tatizo la ndoa za utotoni ndani ya jamii.

Aidha, mabinti kuhudhuria kwenye ndoa za kimila au bukwilima ili kuhamasisha mabinti kujamiiana na marafiki wa bwana harusi ili kupata bahati ya kuolewa sasa hivi halipo tena baada ya juhudi za kuielimsha jamii.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA NASRA SERENY,
UDOM

# Vijana wakizibaini tamu, chungu za mitandao ya kijamii watafanikiwa

WENGI ukiwauliza iwapo mitandao ya kijamii ni kitu muhimu kwa jamii, jawabu lao ni ndiyo kwa sababu ya kuchochea maendeleo na mabadiliko ya kiteknolojia, japo kuna baadhi wanasema imechangia mmomonyoko wa maadili.

Huenda wote wapo sahihi na hii ni kwa sababu kuna athari kama mitandao hiyo itaachwa ikitumiwa vibaya kuwapotosha watoto.

Watanzania ni miongoni mwa watumiaji wakubwa wa mitandao duniani, ikiwamo ya Facebook, Instagram, Twitter, X na Whatsapp kwa ajili ya kufanya biashara, elimu, teknolojia, tiba na burudani.

Wapo wanaoitumia kwa mitandao hiyo vibaya, hususani vijana baada ya kuhitimu elimu ya sekondari na kuwa janga kwa taifa.

Badala ya kutumia simu hizo kupitia mitandao hiyo kujifunza mambo mbalimbali yanayoendelea duniani, kipaumbele chao ni kuangalia picha za ngono, uhalifu na mambo mengine ambayo hayaonyeshwi hadharani ili kutunza siri na utu wa mtu.

Kuna wanaotumia simu na mitandao hiyo kutapeli watu kwenye mtandao wa facebook na instagram. Baadhi hujifanya wanauza bidhaa mbalimbali kama simu na nguo na kumtaka mteja kutuma fedha za kununua na kusafirisha bidhaa.

Baada ya kutuma fedha, unakuwa mwisho wa mawasiliano kati ya mfanyabiashara huyo na mteja wake.

Vilevile kuna wengine hujifanya wanasiasa, viongozi wa serikali, watu mashuhuri ambao wamekuwa wakiomba michango ya fedha kwa kuchangisha watu au wafuasi wao kwa kutumia mitandao hiyo kwa njia ya utapeli.

Matumizi mengine mabaya yanayoonekana kushika chati ni kutupia picha za utupu kwenye mitandao hiyo, ambazo zinaweza kushawishi watoto wadogo kujiingiza katika vitendo hivyo na kuchangia mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Picha hizo ni pamoja na zile za 'kujiposti' mtu akiwa amevaa nguo nusu uchi, mavazi yanayoonyesha maumbile, kuvuta bangi, shisha na kunywa pombe kali hadharani.

David John, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), anasema ameanza kutumia simu janja ambayo alipewa zawadi na wazazi wake baada ya kufaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2014.

Anasema kwa kipindi hicho, mtandao wa kijamii uliokuwa unatamba duniani ulikuwa ni facebook na kwamba alikuwa akitumia kuwasiliana na marafiki zake aliosoma nao tangu chekechea.

Anasema baadaye alijiunga na instagram alipofika kidato cha nne mwaka 2018 hadi cha sita 2021 na kwamba matumizi yake ni ya kawaida si kama zamani: " Siku hizi nimejikita zaidi kujisomea na kufanya biashara, nikiingia mtandaoni ni kujitangaza zadi kibiashara na si vinginevyo," anasema.

Mwanafunzi wa Taasisi ya Uhasibu (TIA), Suzan Mwakajonga, wa mwaka wa pili wa shahada ya usimamizi wa biashara anasema ameanza kutumia simu janja baada ya kuhitimu kidato cha nne mwaka 2018.

Anasema tangu kipindi hicho, anatumia mitandao ya telegram na Instagram kuuza nguo.

"Kwa kuwa bado sijafungua duka, natumia muda mwingi kuposti picha kwenye kurasa zangu za biashara za 'kifuna stores' na 'kifuna jeans' kuwasiliana na wateja wangu," anasema na kuongeza:.

"Bila mitandao ya kijamii nisingekuwa napata muda wa kusoma na kuendesha biashara ya mtandaoni kwani ingenibidi kuwa kama machinga au nitafute duka la kusimamiwa muda wote. Kwangu mitandao ya kijamii imenisaidia sana kusonga mbele kuliko kuniaathiri kimaisha."

Monica Gabriel (22), anasimulia kuwa mtoto wake alitapeliwa Shilingi 330,000 mwaka jana baada ya kudanganywa kuwa anauziwa simu aina ya I phone kutoka Zanzibar.

Anasema alitakiwa kutuma fedha nusu kwa ajili ya kusafirisha simu hiyo kwa makubaliano angemaliza kiasi kilichobaki baada ya kupokea 'mzigo'.

"Ni uzembe wa binti yangu, siyo rahisi mtu atume bidhaa na atake pesa nusu bila kukupa mawasiliano ya jina la kampuni na taarifa sahihi, vijana wengi wanachukulia poa hii mitandao na wanaamini watu kwa urahisi," anasema na kusisitiza kuwa: " Serikali inabidi iingilie kati na kukomesha wizi na utapeli wa mitandaoni."

Kwa ujumla mitandao hurahisisha kupata taarifa kwa haraka na kuinua vipaji hasa kwa vijana kuanzia wanamuziki, wabunifu na wafanyabiashara.

Pia, mitandao hiyo imefanikisha kuibua ajira mpya na kutangaza nafasi za kazi katika jamii na endapo itatumiwa vibaya na vijana madhara yake yanaweza kuwa mabaya ikiwa ni pamoja na kushtakiwa.



Vijana hutumia mitandao ya kijamii 'kuposti picha za 'selfii' hata kama hawapati faida. **PICHA: MTANDAO**

## Kutumia mabibi harusi feki mbinu inayobuniwa kukwepa rungu la dola

**INATOKA UK.11**

Mzee maarufu kutoka Masengwa Juma Ngelela, anasema katika mapambano hayo ya kutokomeza ndoa za utotoni, elimu inahitajika zaidi, ikiwamo na wazazi kuacha tabia ya kuwaogesha watoto wao na dawa za mvuto wa mapenzi.

"Kwa kiasi fulani jamii imepata elimu juu ya madhara ya kuozesha watoto, lakini hamasa hiyo inahitaji kuwa endelevu pamoja na sheria ndogo kutiliwa mkazo, mzazi akikamatwa anaozesha mtoto awajibishwe ipasavyo,"anasema Ngelela.

Mwenyekiti wa Baraza la Watoto Mkoa wa Shinyanga na Taifa, Raphael Joseph, anawasihi wazazi na walezi kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kuwapatia haki zao za msingi, ikiwamo kuwapeleka shule na kuacha kuwabagua watoto wa kike na kuwaozesha ndoa za utotoni.

Anawataka watoto wanapoona viashiria vya kufanyiwa ukatili, watoe taarifa mapema kwa viongozi wa mabaraza ya watoto, walimu hata viongozi serikali za mitaa ili hatua za haraka zichukuliwe na kuzuia vitendo vya ukatili zikiwamo na ndoa za utotoni.

Mkurugenzi wa Shirika la WEADO ambalo linatetea haki za watoto, wanawake, na wazee mkoani Shinyanga, Eliasenya Nnko, anasema katika mapambano ya kutokomeza ndoa na mimba za utotoni wilayani Shinyanga, wanatekeleza mradi wa 'Vunja Ukimya Zuia Ndoa na Mimba za Utotoni', kwa kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara ya kuozesha watoto.

Anasema ili kutokomeza tatizo hilo la ndoa za utotoni jamii inapaswa kuelewa madhara ya kuozesha watoto katika umri mdogo, ndiyo maana kwa sasa wapo katika utekelezaji wa mradi wa kutoa elimu kwa wananchi ya kuacha vitendo vya ukatili ikiwamo kuozesha watoto na kuzima ndoto zao.

Kwa mujibu wa Takwimu zilizotolewa na Shirika la watoto Duniani (UNICEF) mwaka 2012, Shinyanga umetajwa kuongoza kwa tatizo la ndoa za utotoni kwa asilimia 59 ikifuatiwa na Tabora 58 ya tatu ni mara 55.

ELIMU

NA CLAUDIA KAYOMBO, SINGIDA

# Ufugaji unavyowatoa vijana baada ya VETA kuwaanzishia program 'spesho'

NI dhahiri kuwa sekta ya ufundi inaelekea kupiga hatua kubwa kila kukicha, ni baada ya serikali kuanzisha Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA), karibu kila kona ya taifa hili.

VETA kuna wataalamu wa fani mbalimbali ikiwamo ya ufugaji, upishi, kilimo, mitambo, urembo, utalii, magari na ushonaji kwa uchache na hapo wanatoa maarifa kwa watu wa rika, ujuzi na viwango tofauti vya elimu kupitia kozi fupi na ndefu.

Singida ni moja ya mikoa ambayo ufugaji ni tegemeo, na mafunzo ya VETA kwenye tasnia hiyo yamefanikisha kupiga hatua katika kipindi hasa cha muongo mmoja baada ya VETA Singida kuanzisha kitengo cha ufugaji huku mafunzo yakihusu 'Afya ya Wanyama na Uzalishaji' yaliyoanzishwa mwaka 2012.

Kozi ya ufugaji inachochea mabadiliko ya kiuchumi kwa kuwa wahitimu hujiajiri na wengine kuajiriwa serikalini na katika taasisi binafsi hivyo kuboresha pato lao na la taifa.

Mkuu wa kitengo cha ufugaji cha VETA Singida, Hamisi Msangi, anasema wakati chuo kinaandaa kozi hiyo mwaka huo, kilianza kwanza na kuuza vyakula vya mifugo hususani kuku.

Anasema awali wafugaji wengi wa kuku wa kienyeji mkoani hapo hawakufuga kwa tija kwani ndege hao walikuwa wakiachiwa kujiokotea wenyewe vyakula au kuwapa mlo wa aina moja hasa mahindi au mtama.

"Kwa sababu Singida inasifika kwa ufugaji wa kuku wa kienyeji, tulianza na kuwauzia wafugaji vyakula kwa bei nafuu huku tukiwapa elimu ya umuhimu wake kwa mifugo yao. "Tuliona tuwape elimu baada ya kubaini kuwa wengi hawakuwa na utaratibu wa kuwapa lishe bora wanyama hao, sana sana waliwalisha aina moja ya chakula".

Anaongeza kuwa vyakula vya VETA vilikuwa na virutubisho vinavyohitajika kwa ukuaji wa kuku na mazao bora, hivyo waliwashawishi wafugaji kufika chuoni kupata mafunzo ya muda mfupi ili kuwawezesha kuendesha ufugaji wenye tija na kwamba mwitikio ulikuwa mkubwa.

Msangi anasema kwa sababu wengi walikuwa wanafuga kwa mazoea, program hiyo imefanikisha kuanza kununua vyakula vyenye virutubisho kwa ajili ya kuku wao, wengine hutengeneza wenyewe baada ya kupata elimu.



Wanafunzi wa VETA Singida wakijifunza utaalamu wa malisho na tiba za mifugo. **PICHA: CLAUDIA KAYOMBO**

"Maeneo mengi sasa wafugaji wanafuga kibiashara, wanatengeneza vyakula bora kwa ajili ya kuku au wananunua kutoka katika kampuni mbalimbali zinazozalisha vyakula vya mifugo," anasema.

Msangi anabainisha kuwa elimu hiyo imechochea mapinduzi katika sekta ya ufugaji hususani wa kuku kwani wengi wanafuga kwa tija na hivyo kupata pato linaloboresha maisha ya familia zao. Anasema mwanafunzi hujifunza pamoja na mambo mengine, vyakula bora vya wanyama lakini pia namna ya kutibu mifugo hiyo.

Chuo hicho hakitoi mafunzo ya ufugaji kuku pekee bali ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, sungura, bata maji na bata mzinga, kwa mujibu wa maelezo yake.

Aidha, kipo katika mchakato wa kuanzisha ufugaji wa kwale, kuendeleza ufugaji wa kanga, bata bukini pamoja na ndege wengine ambao hawapo kwa sasa chuoni hapo, lengo ni kuwawezesha wanachuo kufahamu tabia zao na namna ya kuwafuga ili baada ya kuhitimu wakaendeleze maarifa hayo wakiwa na uhakika wa kile wanachokifanya, anasema mkuu wa kitengo cha ufugaji VETA Singida, .

Licha ya kujifunza afya ya wanyama na uzalishaji, Msangi anasema wanafunzi wanajifunza progamu za uchakataji maziwa ili kuyaongezea thamani.

"Kuna kiasi tunachakata mtindi, pia tuna jengo jipya la maabara ambalo tunatarajia litafunguliwa kuanzia mwakani, tukitarajia kupata vifaa vya kitaalamu ambavyo vitatuwezesha kupima magonjwa ya mlipuko ya mifugo iliyoko ndani na nje ya chuo ili kubaini chanzo chake na tiba kwa haraka," anasema Msangi.

Mwalimu Ladislaus Chemele wa idara hiyo, anasema mwanafunzi awapo mafunzoni anapata fursa ya kujifunza namna bora ya kufuga nguruwe, sungura na ndege kama kuku na namna ya kuwatibu. Anasema elimu hiyo ni mtaji kwa mhitimu kwa sababu hata asipopata ajira anajiajiri kwa sababu anajua namna ya kumtunza mnyama ikiwa ni pamoja na kuangalia mwenendo wa afya yake.

"Licha ya kufundisha darasani pia kuna wakati chuo kinawatembelea wafugaji ili kuwapa maarifa ya namna ya kufuga kwa tija. Mara nyingi tunawafikia wanaofuga ng'ombe wa kisasa, namna mfugaji anavyowatunza wanyama wake, nasi tukiwa na wanafunzi tunampa maarifa ya namna ya kufuga kwa tija zaidi."

Aidha, wanawafundisha wanafunzi namna ya kufuga kitamaduni, akieleza kuwa wafugaji wengi wanaofuga ng'ombe kienyeji hawana utayari wa kuelimishwa namna ya kuendeleza ufugaji wenye tija.

Akijibu kuhusu idadi ya wanaSingida waliofikiwa na chuo anasema "Ukimwelimisha mtu mmoja umeelimisha wengine 10 ambao atawapa elimu".

Hivyo, kwa wale waliopata elimu hiyo ana uhakika kuwa wameieneza kwa wenzao wengi na hivyo jamii kubwa ina elimu kuhusu ufugaji wa aina mbalimbali.

Mwanafunzi Ridhaael Munuo wa mwaka wa kwanza katika fani hiyo anasema anajisikia fahari kubwa kuchukua maarifa yanayohusu ufugaji kwani licha ya kuwa yupo mwaka wa kwanza lakini amebaini kuwa mafunzo kuhusu wanyama ni mazuri mno.

Anaamini iwapo vijana wengi wakijikita kutafuta maarifa kuhusu utunzaji wa wanyama suala la ajira kwao halitakuwa tatizo.

Halikadhalika, mfugaji Isack Evodi mkazi wa Mwenge, mjini hapa, anaishukuru VETA Singida kwa kubadilisha maisha yake, akisema anajivunia elimu akiwawashauri wafaugaji kutafuta mafunzo, Kaimu Mkuu wa Chuo, Alphoncina James, anatoa wito hususani kwa wakazi wa Singida kujitokeza kwa wingi kusoma kozi mbalimbali za muda mfupi na mrefu zinazotolewa hapo chuoni.

Alphoncina anasema chuo kimejipanga kupokea idadi ya wanachuo wengi ili kuwapa maarifa wayatakayo ili kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Anasema licha ya mkakati na dhamira nzuri ya serikali ya kuanzisha VETA ili kutoa fursa kwa wahitimu kujiajiri na kuajiriwa bado kuna mwitikio mdogo kwa wananchi wa Singida kujiunga na kozi mbalimbali zinazotolewa na chuo hicho kwa kuwa wengi wanatoka mikoa mingine.

Anaweka mkazo kwa wananchi kutumia fursa ya kuwapo chuo hicho kujipatia maarifa yatakayowawezesha vijana wengi kujiajiri au kuajiriwa.

"Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya teknolojia, vifaa vya kujifunzia navyo vinatakiwa viwe vya kisasa zaidi, niiombe serikali kama bajeti itaruhusu ilete vifaa mbalimbali vya kisasa kwa ajili ya kujifunzia katika fani mbalimbali ikiwamo ya ufugaji," anasema Mkuu wa Chuo cha VETA, Singida.

Aidha, anatoa wito kwa Watanzania kuchangamkia kozi fupi katika chuo hicho ambazo zinawapa wahitimu maarifa ambayo yanawawezesha kujiajiri au kuajiriwa.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Maisha mapya kwenye mwezi ni dhahiri baada ya kuthibitika kuwa maji yapo

CHANDRAYAAN-3 chombo cha India kilichokwenda mwezini karibuni, kimefichua ufahamu mpya wa eneo la kusini la mwezi.

Nchi kama Marekani, China na Urusi, zimepanga kutuma ujumbe wake baadaye, lakini ni nini kinachofanya eneo hili liwe na mvuto zaidi kuliko kaskazini?


Wiki iliyopita, chombo kidogo cha rover cha Pragyaan kutoka Shirika la Utafiti wa Anga la India (ISRO), kilitua chini mwezini kutoka kwenye, Vikram lander ya India pia na kuanza kuchunguza eneo karibu na ncha ya kusini ya mwezi.

Wakati safari za Apollo za miaka ya 1960 na 70 hazikugusa kizio cha kusini, lakini safari ya ujumbe wa Chandrayaan-3 ya India ilifanikiwa kugusa maili 370 (kilomita 600) kutoka kwenye nguzo ya kusini ya mwezi, kikiwa cha kwanza kufika eneo hilo.

Chombo hicho kilifika kwa kishindo baada ya jaribio la Urusi kulifikia eneo hilo kushindwa siku mbili kabla, ambapo chombo cha anga za juu cha Luna-25, kilishindwa kujidhibiti na kuanguka. Ujumbe wa India ni mwanzo wa shughuli za haraka katika sehemu hi ya ajabu ya uso wa mwezi ambayo hatimaye itashuhudia wanadamu wakiweka mguu huko miaka michache ijayo.

"Ni jambo la kushangaza kwamba hili linatokea," anasema Simeon Barber, mwanasayansi wa sayari katika Taasisi ya Open University nchini Uingereza.

Kando na India na Urusi, Marekani na China zinatarajia kufika kwenye ncha ya kusini ya mwezi, kuchunguza baadhi ya siri za kuvutia zaidi za mwezi na labda hata kutumia kile wanachopata.



Ncha ya kusini ya mwezi kama inavyoonekana katika ramani, rangi nyekundu inaonyesha ardhi ya juu na zambarau ni eneo chini ya ardhi. **PICHA: KITUO NASA**

### KUNANI KUSINI

Tayari Chandrayaan-3 na rover yake ya ukubwa wa sanduku dogo (suit caise) wamerudisha vidokezo vichache vya kuonyesha mazingira ya ajabu wanayoyashuhudia.

Kusafiri kwa karibu sentimita moja kila sekunde kwenye sakafu ya vumbi, rover ya Pragyaan imejifunga mita kadhaa kutoka kwa chombo kilichoileta.

Kwa kurusha ving'amuzi vya taarifa zake kwenye udongo wa mwezi njiani, rover imefichua kushuka kwa joto kali chini ya uso wa mwezi.

Katika uso wa mwezi chombo hicho kilirekodi joto la karibu nyuzi 50 (120F), lakini inchi tatu hali ya joto ilishuka kwa -10C (14F) tofauti ya joto ambayo imewashangaza wanasayansi.

> "Mhimili wa mwezi wa mzunguko, ni nyuzi 1.5 ikilinganishwa na nyuzi 23.5 za dunia, inamaanisha kuwa baadhi ya maeneo ya nguzo zake hayapati mwanga wa jua.

Vifaa vya uchambuzi wa kemikali pia vimeonyesha uwepo wa salfa, aluminium, kalshamu, titaniam, manganizie, kromiam na oksijeni katika udongo wa mwezi.

Matokeo haya yote ya awali yanaonyesha ni kwa nini wanasayansi wana hamu ya kuchunguza eneo la kusini la ncha ya mwezi.

Mhimili wa mwezi wa mzunguko, ni nyuzi 1.5 ikilinganishwa na nyuzi 23.5 za dunia, inamaanisha kuwa baadhi ya maeneo ya nguzo zake hayapati mwanga wa jua.

Pamoja na joto la chini katika maeneo haya, wanasayansi wanaamini hii imesababisha wingi wa barafu, mengi ya hayo ambayo mengi yana maji, ambayo ni au yamechanganyikana na udongo ama yanayoonekana wazi juu ya uso wa mwezi.

Kuna matumaini kwamba barafu inaweza kutumika kama rasilimali kwa wanaanga na kwa ajili ya uvumbuzi wa kisayansi wa baadaye.

"Ni eneo la kipekee," anasema Saumitra Mukherjee, profesa wa jiolojia katika Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru cha New Delhi, India. "Upatikanaji wa maji ni muhimu sana."

Wakati mwingine huitwa "craters ya giza la milele", maeneo yenye kivuli miale ya jua hailifikii, ikimaanisha kuwa yamehifadhi barafu kwa mabilioni ya miaka.

Ushahidi wa barafu ya maji mwezini unatokana na jaribio la NASA la Oktoba 2009 wakati roketi tupu ilipigwa kwa makusudi kwenye crater katika ncha ya kusini. "Sampuli za vifaa ilikuwa na ushahidi wa maji," anasema Margaret Landis, mwanasayansi wa sayari katika Chuo Kikuu cha Colorado, Boulder, nchini Marekani. "Huo ni uchunguzi wetu wa moja kwa moja wa barafu ya maji kwenye mwezi."

Takwimu nyingine zinaonyesha kutafakari juu ya nguzo, matokeo ya uwezekano wa barafu, wakati kiasi kikubwa cha haidrojeni kwenye nguzo kimezingatiwa, labda matokeo ya barafu ya maji.

Mwaka jana mwanasayansi William Reach katika kituo cha utafiti cha Ames cha NASA cha California alirusha darubini katika ndege ya kuchunguza mwezi, na kupata ushahidi wa hidrojeni "nje tu" eneo la kutua ambalo sasa linamilikiwa na Vikram ya Chandrayaan-3 na rover yake tangu walipotua mwezi uliopita.

Uvumbuzi huu wa hivi karibuni wa barafu ya maji umechochea hamu mpya ya kuchunguza mwezi, na hasa, ncha yake ya kusini.

Chombo cha Chandrayaan-3 na rover ya India sasa vitaruhusu wanasayansi "kupima nadharia ambazo watafiti wa mwezi wamekuwa wakizitaja kuhusu uwepo wa barafu katika udongo wa mwezi," anasema Aanchal Sharma, mhandisi wa zamani katika Shirika la Utafiti wa Anga za Juu la India (ISRO), sasa akifanya kazi katika Chuo Kikuu cha Trento, Italia.

Wakati data za Chandrayaan-3 zitakuwa muhimu, ni baadaye ujumbe ambao utatua karibu na ncha ya kusini ambayo wanasayansi wataifurahia zaidi.

Hapa, kuna eneo la maji linalojulikana kama kanda ya kivuli kabisa (PSRs). Wakati mwingine huitwa "makaburi ya giza la milele", miale ya jua haifikii sehemu zake, ikimaanisha kuwa yamehifadhi barafu kwa mabilioni ya miaka.

Ncha ya kusini ina maeneo ya maji zaidi kuliko kaskazini, uwezekano wa matokeo ya athari ngapi za hali ya hewa zimegonga uso, na kufanya kizio cha kusini kuwa lengo la kuvutia zaidi.

Hizi sio safari pekee zinazolenga ncha ya kusini ya mwezi. Ujumbe wa India kwa kushirikiana na Japan, Chandrayaan-4, pia utaelekea huko, wakati China imeashiria nia yake ya kutua katika eneo hili na Urusi ina pia mpango mwingine kufika katika nchi ya kusini.

Maji ya barafu ndiyo yanayochochea safari hizi. Iwapo yapo kwa wingi na yanapatikana yanaweza kuwa rasilimali muhimu kwa makazi ya binadamu kwenye mwezi na uchunguzi zaidi katika mfumo wa jua.

Ikiwa barafu inaweza kuchukuliwa kutoka kwenye udongo wa mwezi inaweza kugawanywa katika hidrojeni na oksijeni, sehemu muhimu ya mafuta ya roketi au chanzo cha maji ya kunywa na oksijeni kwa binadamu watakaokwenda huko. Ndoto hizi za kusafiri kwa kina na kuishi mwezini ni karibu kuliko mtu anavyoweza kufikiria. **BBC**



## ATE yahimiza waajiri kuzingatia sheria za nchi

**Na Renatha Msungu,**DODOMA

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), kimewataka waajiri wote nchini kufuata Sheria za Ajira na Uhusiano Kazini ya Mwaka 2004, inayoweka bayana miongozo, wajibu na majukumu mbalimbali ikiwamo utoaji mikataba kwa wafanyakazi ili kuepuka migogoro.

Mkuu wa Wanachama na Masoko wa ATE, Patricia Chao, aliagiza hayo jana katika mkutano wa waajiri na wadau wa Kanda ya Kati uliolenga kujadili sheria za kazi na utendaji bora.

Chao alisema kuwa ili wafanyakazi wafanye kazi kwa ufanisi na weledi, miongozo ya kazi inapaswa kuwekwa bayana kwa kuwa itachangia kukuza uchumi na kuongeza ufanisi na tija mahala pa kazi.

Alifafanua kuwa ili kuepuka migogoro mahala pa kazi, ni muhimu waajiri kufuata sheria za kazi kama zinavyoagiza ili kuepuka kesi ambazo huharibu sifa ya kampuni na wafanyakazi wake kwa ujumla.

"Ninaomba ninukuu kesi ya mwaka 2022 katika Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kati ya mwajiri na mfanyakazi, ambapo mwajiri hakuwahi kutoa mkataba kwa madereva na baadae akaamua kumwondoa kazini mmoja wa wafanyakazi wake, ndipo akafunguliwa kesi ya kuvunjiwa mkataba wa ajira.

"Dereva aliamini kuwa mkataba wake kila mwaka unahuishwa moja kwa moja. Hivyo, siku mwajiri alipomwachisha kazi dereva alikwenda kufungua mashtaka.

"Iliamuliwa kuwa mwajiri amlipe mfanyakazi wake (Dereva) mishahara yake yote kwa kile kipindi kilichobakia kwa kuzingatia masharti ya kipindi kilichopita," alisema.

Kiongozi huyo alisema ATE, moja ya kazi yake ni kuhakikisha inasaidia waajiri kwa kutoa mafunzo, ushauri na kuwaongoza katika kutekeleza sheria hizo kwa maanufaa ya kampuni zao na taifa kwa ujumla.

Mwanasheria Emmanuel Miage, alisema waajiri na waajiriwa ni vyema wakatambua haki na wajibu wa kila mmoja ikiwamo haki ya kusikilizwa kwenye jambo lolote linalomkabili kabla hajachukuliwa uamuzi kupitia sheria zilizoelekezwa.

Alisema ATE hufanya kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA).

Ofisa Miradi Mkuu kutoka Sightsavers Tanzania, Sabina Maheke, alisisitiza mabadiliko juu ya dhana ya watu wenye ulemavu ikiwamo uelewa kwa jamii juu ya ulemavu, waajiri kuwaamini na kuwaajiri na walemavu wenyewe kujikubali na kuthubutu kushiriki katika kuzipambania ndoto zao katika ajira na kujiajiri.

Alisema lengo namba nane katika Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, linahimiza ukuaji wa kiuchumi unaohusisha watu wote na endelevu.

**"Iliamuliwa kuwa mwajiri amlipe mfanyakazi wake (Dereva) mishahara yake yote kwa kile kipindi kilichobakia kwa kuzingatia masharti ya kipindi kilichopita," alisema.**

# Waziri aonya hujuma ujenzi wa barabara

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ameonya wananchi watakaopitiwa na mradi wa ujenzi wa barabara ya Sabasaba-Sepuka-Ndago-Kizaga mkoani Singida yenye urefu wa kilometa 77.6, kujihusisha na hujuma yoyote ikiwamo wizi wa vifaa ili ujenzi huo ukamilike kwa thamani iliyopangwa.

Bashungwa alionya hayo jana katika hafla ya kumkabidhi Mkandarasi Henan Highway Engineering Group Ltd toka China kuanza kazi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Ni mradi unaogharimu Sh. bilioni 88.

"Serikali imetoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini ikiwamo Mkoa wa Singida. Niwapongeze wananchi kwa ushirikiano mnaowapa makandarasi.

"Hata hivyo, nitoe tahadhari ya wizi wa mali na vifaa vitakavyotumika katika ujenzi. Ninaomba viongozi wasisitizeni wananchi wanaozunguka maeneo ya mradi kuepukana na uhalifu wa aina yoyote wa vifaa," alisema.

Bashungwa aliagiza Wakala wa Barabara (TANROADS) kuhakikisha unamsimamia kikamilifu mkandarasi huyo na kukamilisha kazi hiyo kwa wakati uliopangwa na kwa ubora.

"TANROADS ndio wenye dhamana ya kusimamia ujenzi wa barabara nchini, jipangeni vizuri ujenzi ukamilike ndani ya muda uliokusudiwa na kwa ubora na si vinginevyo," alisema.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwataka Watanzania kuwa wamoja hasa katika kuinua uchumi wa nchi, kazi ambayo serikali imeianza kwa kushirikisha sekta binafsi.

"Mimi kitaaluma ni mchumi, hakuna nchi yoyote duniani ambayo inaweza kukuza uchumi wake pasipo kuwekeza kwenye sekta binafsi na katika jambo hili, hatutarudi nyuma kwa kuwa litaongeza mapato ya nchi na kutuwezesha kutoa ajira nyingi, ikiwa ni pamoja na za wauguzi ambao watakuwa wakifanya kazi kwenye vituo vingi vya afya tulivyovijenga nchi nzima," alisema Dk. Mwigulu.

Alisema kumekuwa na tofauti katika jambo hilo la uwekezaji hadi kufikia hatua ya kutaka kufarakana kati yao. Anaamini kupitia uwekezaji, watapiga hatua na wenzao ambao hawautaki wakidai serikali inaweza kufanya kazi hiyo peke yake.

Dk. Mwigulu alitumia nafasi hiyo kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa serikali kutoa fedha za ujenzi wa barabara hiyo ambayo alikuwa ameanza kuiomba tangu alipoingia bungeni kwa mara ya kwanza.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema katika kipindi cha miaka miwili ya utawala wa Rais Samia Suluhu Hassan, mkoa umepewa Sh. bilioni 210 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya barabara.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima, akiwa kwenye pikipiki zilizokabidhiwa kwa wanawake wajasiriamali kupitia programu ya IMBEJU katika uzinduzi wa maonesho ya wajasiriamali yanayoendelea viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. Wengine pichani ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa (kulia), Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (wa tatu kulia) na Mkurugenzi wa BUTA VICOBA Endelevu, Semeni Gama (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Vijana acheni kulalamika, ajira ziko shambani, zizini'

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana (UVCCM) Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma, amewataka vijana kuwekeza katika kilimo, uvuvi na ufugaji ili wajiajiri wenyewe na kuajiri wenzao badala ya kuendelea kuinyooshea vidole serikali kwa kukosa ajira.

Justen Sangulah alitoa rai hiyo juzi alipozungumza katika kikao cha Baraza la Vijana.

Alisema kuwa badala ya kusubiri serikali itoe ajira, vijana wanatakiwa kujikita katika kilimo, uvuvi na ufugaji ambao utawawezesha kujiajiri wenyewe na kuajiri vijana wenzao.

"Wilaya yetu ya Bahi ina sifa ya kuwapo sekta mbalimbali ambazo zinazoweza kubadilisha vijana kimaendeleo na kiuchumi. Hivyo, ninawaomba badala ya kusubiri ajira kutoka serikalini ni vyema wakajikita katika fursa hizo ambazo zitawabadilisha maisha yao," alisema.

Sangulah pia aliwataka vijana wa wilaya hiyo kuiunga mkono serikali kwa juhudi zinazofanywa katika kuliletea Taifa maendeleo, pia kukataa kutumiwa na watu wasiotakia mema nchi kwa lengo la kuharibu amani.

Akifungua kikao cha baraza hilo, Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo, aliwataka kuungana kuanzisha vikundi vitakavyowawezesha kupata mikopo kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali.

Alisema serikali chini ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) iko tayari kuwasimamia kwenye vikundi ambavyo vitaanzishwa kwa ajili ya kuhakikisha wanapata mikopo ambayo itabadilisha mitizamo ya maisha yao.

Pia aliwataka vijana hao kuhakikisha wanajiendeleza kielimu kupitia nafasi walizonazo ili wasimamie wenzao katika sekta mbalimbali zikiwamo za kijamii, kiserikali, kiroho na kichama kwa ujumla.

Aliagiza vijana wa wilaya hiyo kuwa mabalozi wa kuwashawishi wenzao kufanya kazi zinazokubalika ikiwamo za kilimo, uvuvi na ufugaji ambazo zitawabadilisha maisha yao kiuchumi.





# W'biashara wanaonunua mazao shambani waonywa

Na Nebart Msokwa,
MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, imeanza kuwadhibiti wafanyabiashara wanaonunua mazao yakiwa mashambani na kusababisha hasara kwa wakulima na kuipotezea halmashauri mapato.

Badala yake wametakiwa kununua mazao hayo kwenye masoko yaliyoanzishwa na serikali kwenye halmashauri hiyo ili walipe mapato ya serikali na kutumia vipimo halali.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Misana Kwangula, alitangaza marufuku hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa anafungua kikao cha wafanyabiashara na wasindikaji wa mazao mkoani hapa kilichofanyika wilayani humo.

Kikao hicho kiliandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), kujadiliana mambo mbalimbali yanayohusu biashara ikiwamo fursa za masoko ya kimataifa.

Kwangula alisema, baadhi ya wafanyabiashara hao wanatoka nje ya nchi na kuingia kinyemela maeneo ya vijijini na kuanza kununua mazao ya wakulima jambo alilosema siyo sahihi kwa mujibu wa sheria.

Alisema vyombo vya dola vinaendelea na ufuatiliaji wa wafanyabiashara hao ili wakibainika wachukuliwe hatua za kisheria na za kiuhamiaji.

"Wafuate utaratibu wa ununuzi wa mazao, yapo masoko ambayo yamejengwa kwa ajili ya kazi hiyo, sasa wale wanaokiuka wakikamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria," alisema Kwangula.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa endapo watawaona wafanyabiashara hao wakiingia kwenye maeneo yao na kuanza kununua mazao ili wadhibitiwe kwa kuwa ndio waathirika wakubwa wa biashara hizo.

Ofisa Biashara kutoka TANTRADE, Chrispin Mathew alisema, serikali inafanya juhudi mbalimbali za kuwadhibiti wafanyabiashara hao wa kutoka nje ya nchi ambao wanaingia bila vibali na kuanza kununua mazao ya wakulima.

Alisema serikali imeanzisha masoko rasmi katika maeneo mbalimbali nchini na kuwataka wanunuzi kutoka nje ya nchi wayatumie masoko hayo ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria.

Alisema viongozi wa nchi za kiafrika walikaa vikao miaka ya karibuni na kukubaliana kuondoa baadhi ya vikwazo vya kibiashara baina ya mataifa hayo, lakini kuna baadhi ya taratibu zinatakiwa kufuatwa.

"Wafanyabiashara hao wanatakiwa kutumia fursa hii ya kuondoa vikwazo vya kibiashara kufanya biashara kwa kufuata taratibu, mtu anayetoka nje ya nchi hatakiwi kuingia moja kwa moja mashambani kununua mazao ya wakulima," alionya Mathew.

Baadhi ya wafanyabiashara walioshiriki kikao hicho walisema kwa sasa biashara ya kimataifa imekuwa ngumu kutokana na kuadimika kwa dola duniani wakieleza kuwa maeneo mengi wanayopeleka mazao wanatakiwa kutumia fedha hizo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Rehema Robert, alisema miaka ya nyuma walikuwa wanatumia fedha za aina yoyote kulingana na taifa wanalopeleka bidhaa, lakini kwa sasa wanatakiwa kutumia dola jambo ambalo limekuwa gumu kwao.

Elia Msuya, alisema biashara ya mazao ina mnyororo wa watu wengi ambao baadhi yao hawatambuliki na serikali na hivyo akataka baadhi yao wadhibitiwe.

Alisema baadhi yao ni madalali na wengine ni wafanyabiashara wa kawaida ambao wananunua mazao kwa wakulima na kuwauzia wafanyabiashara hao wa kimataifa.

Hivi karibuni limeibuka wimbi la wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kwenda kununua mazao ya wakulima mashambani na baadhi yao wamekuwa wakinunua mazao yakiwa mabichi jambo ambalo linadaiwa kuwasababishia wakulima hasara.



Spika wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, akikabidhi msaada wa matofali yenye thamani ya Sh. milioni 24.7 kwa uongozi wa hospitali ambayo yatatumika katika ujenzi wa jengo la upasuaji wa moyo na mishipa ya fahamu katika Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya juzi. **PICHA: MICHAEL MSOMBE**

## Wakulima watarajia tija zaidi uzalishaji mazao

**Na Elizabeth John**, NJOMBE

WAKULIMA wa mazao mbalimbali mkoani Njombe, wamesema wanatarajia kupata tija zaidi kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo msimu ujao tofauti na ilivyokuwa msimu uliopita kutokana na serikali kuweka vizuri mfumo wa mbolea ya ruzuku.

Walisema msimu uliopita ambao ulikuwa wa kwanza serikali kuweka ruzuku, walikuwa wanazipata maeneo ya wilayani, lakini kwa msimu huu wameelezwa kuwa mbolea hizo zitakuwa zinapatikana ngazi ya kata.

Serikali imetangaza bei elekezi ya mbolea ya ruzuku katika msimu mpya wa kilimo 2023/2024 na bei hiyo itatofautiana kulingana na umbali wa kituo cha kuchukulia mbolea.

Akitaja bei hizo, Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya mji Njombe, Henry Kideula, alisema lengo la serikali kutofautisha bei ni kuwawezesha mawakala kufikisha mbolea mpaka vijijini kwenye maeneo ya uzalishaji.

Kideula alisema wastani wa bei ya mbolea ya CAN itakuwa ni kati ya Sh. 59,220 mpaka 59,550, UREA kati ya Sh. 64,220 mpaka 64,550, DAP Sh. 74,221 mpaka 74,551.

Mmoja wa wakulima, Keneth Luhambati, alisema serikali imefanya jambo jema kuweka utaratibu wa kutangaza bei mpya mapema itasaidia wakulima kuchukua mbolea kwa wakati na kuongeza uzalishaji.

"Kwanza tunakwenda kuzalisha mapema kwa sababu tuna kilimo cha umwagiliaji ambacho tunalima kiangazi muda kama huu, hili jambo litatusaidia kwa sababu mwaka jana mbolea zilifika kwa kuchelewa," alisema Luhambati.

Meneja wa Kampuni ya Mtewele General Traders, Sady Mwang'onda, ambao ni wakala wakubwa wa mbolea mkoani Njombe, alisema tayari wameshaanza kusambaza mbolea kwa wakulima huku akipongeza mfumo wa sasa.

"Ukiangalia kwa msimu uliopita kulikuwa na bei inafanana kwenye maeneo yote,kwa hiyo ilikuwa inatupa changamoto kidogo kwasababu ilituhitaji tufikishe mbolea hizi kwa wakulima kule vijijini ambako wakulima wanalima, lakini bei ilikuwa inafanana na kutupa shida kwenye gharama za usafirishaji," alisema Mwang'onda.

Akizungumza kwa njia ya simu, Diwani wa Kata ya Yakobi, Halmashauri ya Mji Njombe, Michael Uhahula, alisema uamuzi wa serikali ni kufikisha mbolea hadi kwenye kata kuongeza kiwango cha uzalishaji kwa wakulima.

"Tija naiona ni kubwa kwa sababu tukiangalia tangu tumeanza mwaka jana hata kiwango cha mazao mashambani kimeongezeka, ukipita huko vijijini unaona kabisa kiwango cha uzalishaji kimeongezeka," alisema Uhahula.

## Daraja Bonde la Mababu lasaidia kurejesha mawasiliano

**Na Nebart Msokwa,**
KYELA

WAKAZI wa Kata ya Mababu, wilayani Kyela, wamesema ujenzi wa daraja la Bonde la Mababu umesaidia kurejesha mawasiliano ambayo yalikuwa yanakatika mara kwa mara hasa kipindi cha masika.

Tangu mwaka 2020 wananchi zaidi ya 40,000 wa kata nne za Mababu, Ndobo, Makawe na Lusungo walikosa mawasiliano kutokana na daraja walilokuwa wakitumia kusombwa na maji na kukata mawasiliano.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi wa daraja hilo na mbio za Mwenge, wananchi wa kata hizo wamesema walipitia changamoto nyingi wakiwamo shughuli za uchumi kukwama.

Kaunda Mwiganju, mkazi wa kata ya Mababu, alisema kwa muda wa miaka mitatu walikosa mawasiliano na shughuli za kiuchumi ziliyumba baina yao na kata nyingine zinazowazunguka.

Alisema kupatikana kwa daraja hilo kutarejesha uhusiano na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kuishukuru serikali kwa kutatua changamoto hizo.

"Biashara ya mpunga ni kama ilisimama kwa sababu tulibaki kwenye kata yetu bila mawasiliano na maeneo mengine, tunaishukuru serikali kwa kutatua kero hii," alisema Mwiganju.

Elizabeth Faustine, alisema wanafunzi waliokuwa wakitumia njia hiyo walikuwa wakipata tatizo la kutembea umbali mrefu.

"Kwa sasa tunaweza kutembea kata moja na nyingine, wanafunzi wataachana na kero ya kutembea umbali mrefu kwenda shuleni na biashara zitaanza kuchangamka," alisema Elizabeth.

Akitoa taarifa za mradi huo kwa kiongozi wa mbio za Mwenge, Kaimu Meneja wa Tarura wilayani Kyela, Mhandisi Kaimu Mtungata, alisema daraja hilo limegharimu zaidi ya Sh. milioni 161.

Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa, Abdala Shaibu, alisema wameridhishwa na mradi huo akiomba wananchi kulilinda na kulitunza.

"Tunahitaji usimamizi kwenye mradi huu, tumekagua nyaraka tumeridhika nayo, maelekezo tuliyotoa yazingatiwe tofauti na hapo sheria zitachukua mkondo wake kwani zipo taasisi zenye tabia ya kudharau," alisema Shaibu.

# Mkoa Kaskazini kumaliza kero upatikanaji majisafi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduara, amesema Mkoa wa Kaskazini Unguja utaondokana na tatizo la uhaba wa majisafi na salama hivi karibu baada ya wizara yake kutia saini hati ya ushirikiano na Kampuni ya Oman National Energy Centre ya kuimarisha mradi wa maji katika mkoa huo.

Akizungumza baada ya hafla ya utiaji saini huo uliofanyika wizarani kwake, alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa mpango wa serikali katika kuwekeza katika miradi ya maji na kuwataka wakazi wa mkoa huo kuwa tayari kupokea huduma hiyo muhimu. Aidha, hatua hiyo ni utekelezaji wa mpango wa serikali kuwekeza katika miradi ya maji.

"Watu wa Kaskazini Unguja kwa muda mrefu wanalalamikia uhaba wa majisafi na salama hivyo mradi huu utakuwa mwarobaini wa suluhisho la tatizo hilo," alisema.

Alisema serikali ina mipango mizuri ya kuondoa changamoto ya uhaba wa maji katika mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Balozi mdogo wa Oman, Said Al Sinawy, alipongeza Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa kuwapatia mkataba huo na kuahidi kuwa nchi yake itasaidia Zanzibar katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya maji.

Alisema hivi karibuni alikutana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi na kufanya mazungumzo ambayo yamedhamiria kuimarisha huduma mbalimbali za kimaendeleo kidijitali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph Kilangi, alisema Mkoa wa Kaskazini una tatizo la uhaba wa maji kutokana na kukua kwa shughuli za uwekezaji hasa katika utalii, serikali ikaona haja ya kutafuta mbinu mbadala ili huduma hiyo ipatikane kwa uhakika.

Alisema mradi huo umelenga kuboresha miundombinu ya maji kwa mkoa huo na utahusisha maeneo mbalimbali kuboresha miundombinu Mahonda, Machui Kiwengwa na Nungwi kutokana na tatizo la upatikanaji wa maji hasa katika eneo la Nungwi na Kiwengwa yanayosababishwa na ongezeko la uwekezaji.

Katibu Kilangi alisema mradi huo unagharimu Dola za Kimarekani milioni 26 na kampuni hiyo itakuwa na kazi ya kuboresha miundombinu, kuchimba visima na kujenga matangi kwa maeneo yanayohitajika na utakuwa wa muda wa miaka mitano.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya National Energy Center (NEC) ya Oman Abudallah Rashid Ali, alisema watahakikisha mradi huo wanakamilisha kwa wakati na kuomba ushirikiano wa karibu ili kufanikisha malengo ya mradi huo.



Mkurugenzi anayesimamia Chuo cha Sayansi na Uhandisi cha India Kampasi ya Zanzibar, Prof. Preeti Aghalayam, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuanza kutoa elimu visiwani Zanzibar Oktoba mwaka huu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

## Taasisi IITM yatoa fursa kupokea wanafunzi duniani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI anayesimamia Taasisi ya Teknolojia ya India Madras (IITM), Kampasi ya Zanzibar, Prof. Preeti Aghalayam, amesema Zanzibar ina fursa ya kupokea wanafunzi wengi kutoka Afrika na duniani ikiwamo India kujiunga na chuo hicho cha sayansi na uhandisi.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar, alisema, chuo hicho Kampasi ya Zanzibar, itatoa programu mbili za kitaaluma ya, shahada ya sayansi na Shahada ya Uzamili ya Teknolojia ya Data katika Sayansi.

"Tuna waombaji zaidi ya 100 kutoka Afrika Kusini, Kenya, Nigeria, Tanzania Bara, Zanzibar na dunia nzima ikiwa ni pamoja na India," alisema.

Akizungumzia miundombinu hiyo, Profesa Preeti, alisema kuwa programu hizo zitaanza kutolewa Oktoba mwaka huu na chuo hicho kipo Kijiji cha Bweleo, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Alisema Serikali ya Zanzibar imewapa ardhi zaidi ya ekari 200 katika eneo la Fumba ili kujenga miundombinu ya kudumu ya chuo hicho yenye viwango sawa na vilivyo katika kampasi kuu nchini India.

Profesa huyo ambaye ni mwanamke wa kwanza kuongoza chuo cha IITM, alipongeza ushirikiano mkubwa anaoupata kutoka kwa maofisa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar.

"Hii ni hatua muhimu zaidi katika juhudi za kimataifa. Mpango wa kina wa kimkakati ambao unajumuisha kuongeza idadi ya wanafunzi wa kimataifa, kukuza mipango ya shahada ya pamoja na ya ushirikiano na taasisi za kitaaluma za kimataifa," alisema.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, aliwataka Wazanzibari kuitumia fursa hiyo kujiunga na chuo hicho ili kuwa na wataalamu wengi wa masuala ya sayansi na teknolojia.

"Nchi inahitaji kuwa na wataalamu wengi wa masuala ya sayansi na teknolojia hivyo Wazanzibari tusiwe nyuma katika kuitumia fursa hii hasa sisi wanawake tusiogope kusoma masomo ya sayansi ili tusiwachwe nyuma na sayansi na teknolojia," alisema.

# SMZ kujenga kituo kurekebisha vijana utumiaji dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inakusudia kujenga kituo cha kurekebisha tabia kwa vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya huko Pemba ambacho kitakuwa na huduma zote ikiwamo za kazi za vitendo za ujasiriamali.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, wakati akizungumza na watendaji wa wizara hiyo baada ya kutembelea taasisi zilizopo chini yake ikiwamo mamlaka ya kupambana na dawa za kulevya.

Alisema mikakati ya serikali ni kuwapo kwa nyumba zitakazotumika kurekebisha tabia za vijana wanaotumia dawa za kulevya.

Alisema lengo la kuwapo kwa nyumba hizo ni kurekebisha tabia na kuwajengea uwezo vijana kuhakikisha kwamba wanapomaliza muda na kuondoka katika maeneo hayo wanapata ujuzi na uwezo wa kazi za ujasiriamali kwa ajili ya kujiajiri.

Alisema mafanikio makubwa yamepatikana kwa vijana ambao wamekuwa wakiishi katika nyumba za kurekebisha tabia, Kidimni Wilaya ya Kati Unguja na wakipatiwa mafunzo ya vitendo ya ujasiriamali.

Katibu Mkuu Ofisi hiyo, Dk. Omar Dadi Sharjak, alisema tangu kuanzishwa kwa nyumba za kurekebisha tabia kwa vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya mafanikio makubwa yamepatikana ikiwamo vijana kurudi katika familia zao na kufanya shughuli za maendeleo na kuachana na dawa za kulevya.

"Tunashuhudia mafanikio makubwa kwa vijana kuachana na dawa za kulevya kwa wale ambao wanaishi katika nyumba za 'Sober house' huku tukiwapatia ujuzi wa kazi za mikono ambazo hizo lengo lake kutengeneza ajira," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya, Kanali Burhani Nassor Zubeir, alisema mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni endelevu na kuitaka jamii kuwafichua watu wanaofanya biashara hiyo ambao wanaishi na jamii.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuja na sheria iliyoipa nguvu mamlaka hiyo katika mapambano na dawa za kulevya ikiwamo kukamata na kufanya uchunguzi pamoja na kufikisha mahakamani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**PAULINA MBALU NONI,** MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA MAENEO YA MOROCCO - DAR ES SALAAM. YENYE NO: **TAE 500920,** ILIYOTOLEWA MAKAO MAKUU UHAMIAJI DAR ES SALAAM MWAKA : 2023

TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI ILALA NA KUPEWA RB NO : **REF: PHQ/DAR/KIN/10983/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**BOB RICHARD NDASSA , ROBERT NA GODFREY NDAHALWA** wanatangaza kupotea kwa hati ya nyumba yenye namba **32145-DRL** plot no **100 block R Itega** manispaa ya DODOMA. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/11041/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VERDIANA ANTHONY SANGA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI (HAOJUE) yenye namba za usajili **MC 980 CEM** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi

**PHQ/MOR/MOR/1372/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA MJINI**

**KITUO CHA MJINI, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......96/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ATHUMANI JUMA MPANGILE wa MSAMVU**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ALLY ATHUMANI MPANGILE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 15 Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

**Imetolewa leo tarehe 7 mwezi 09 mwaka 2023**

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa wa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1341/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RUKIA MOHAMED MESSO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA FATMA ABDULRAHAMAN**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10 Mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 06 Mwezi wa 09 Mwaka 2023.**

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA VYETI VYA TAALUMA



**SHABANI BAKARI SHABANI** antangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2733-0092** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ITEGA SECONDARY SCHOOL mwaka 2013, pia cheti cha cha kidato cha sita chenye idex namba **S0150-0576** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia TANGA TECHNICAL SECONDARY SCHOOL mwaka 2016 na cheti cha chuo na transcript ya Bachelor of science in Nursing kilichotolewa na **SAINT JOHN'S UNIVESITY OF TANZANIA DODOMA** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **TAARIFA POLISI:DOD/DOD/RB/386489/2022 POLISI TAARIFA: DOD/DOD/RB/386385/2022**

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Mataifa yaipa mkono wa pole Morocco

**MARRAKECH,** Morocco

MATAIFA mbalimbali ulimwenguni ikiwemo Marekani, Israeli, Bara la Ulaya, Mashariki ya Kati, pamoja na mashirika ya umma yametoa msaada nchini Morocco baada ya kukumbwa na tetemeko la ardhi lililosababisha maafa makubwa ikiwemo zaidi ya watu 2,500 kupoteza maisha.

Morocco ilikumbwa na tetemeko la ardhi la nyuzi 4.5 kwenye kipimo cha Richter, mwishoni mwa wiki iliyopita na kusababisha madhara kwa wananchi ikiwemo kuharibu makazi, usafiri, miundombinu ya nyumba na barabara.

Pia ilielezwa kuwa waokoaji wanaendelea na zoezi la kutafuta manusura waliokwama chini ya vifusi katika vijiji vilivyokumbwa na tetemeko hilo, hali ambayo imeyalazimu mataifa mbalimbali kufikia uamuzi wa kutuma misaada ya kibinadamu nchini Morocco.

**Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, ambaye alisema janga hilo linawaathiri wao wote, alieleza kwamba Paris imekusanya timu zote za kiufundi na usalama ili kuweza kuingilia kati wakati mamlaka ya Morocco itaona kwa ni muhimu.**

### MAREKANI

Naibu Mshauri wa Usalama wa Kitaifa wa Marekani, Jon Finer, alisema nchi yake imeiambia serikali ya Morocco kwamba iko tayari kutoa msaada muhimu.

"Tuna timu za utafutaji na uokoaji zilizo tayari kutuma wafanyakazi wake na pia tuko tayari kutoa fedha kwa wakati unaofaa ili kuwasaidia Wamorocco wasiweze kukata tamaa na kukabiliana na janga hili la kutisha," alisema.

### ULAYA

Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, ambaye alisema janga hilo linawaathiri wao wote, alieleza kwamba Paris imekusanya timu zote za kiufundi na usalama ili kuweza kuingilia kati wakati mamlaka ya Morocco itaona kuwa ni muhimu," alisema.

Ilielezwa kuwa timu ya wazima moto wa kujitolea wa Ufaransa kutoka eneo la Lyon tayari wamewasili Morocco juzi na watashiriki katika shughuli za uokoaji karibu kilomita hamsini kutoka Marrakech, kulingana na mamlaka ya mkoa huo.

Wizara ya Ulinzi ya Uhispania ilisema imetuma timu ya waokoaji 56 nchini Morocco baada ya kupokea ombi rasmi la usaidizi kutoka Rabat. Na kwamba ndege ya kijeshi ya A400 iliruka kutoka kambi ya Zaragoza ikiwa na timu hiyo kuelekea Marrakech ili kusaidia katika uokoaji wa manusura," ilisema.

Kitovu cha tetemeko hilo la ardhi, la ukubwa wa 6.8 kwenye kipimo cha Richter kulingana na Taasisi ya Marekani ya Jiofizikia (USGS), kinapatikana Kusini Magharibi mwa Marrakech, kilomita 320 Kusini mwa mji mkuu Rabat.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Uswizi, ilisema ilijitolea kutoa makazi ya muda, vifaa vya kutibu na usambazaji wa maji, vifaa vya usafi wa mazingira na vifaa vya usafi. Ikielezwa kuwa uwasilishaji wa vifaa hivyo utaambatana na wataalam kutoka Shirika la Misaada ya Kibinadamu la Uswisi (CSA).

Ulinzi wa Ubelgiji ulitangaza kuwa huduma ya uratibu wa misaada ya dharura nje ya nchi (B-Fast) ilianzishwa ili kujibu maombi ya usaidizi kutoka kwa mamlaka ya Morocco.

Italia pia ilitoa msaada kutoka kwa kikosi chake cha ulinzi wa raia na wazima moto, huku Kanisa Katoliki la Italia likituma euro 300,000 kupitia shirika la Caritas Italia.

Rais wa Italia, Sergio Mattarella, alisema nchi hiyo iko tayari kuchangia kazi ngumu ya uokoaji.

Uturuki ilipendekeza kutumwa kwa waokoaji 265 na mahema 1,000, bila majibu kutoka mamlaka ya Morocco.

Naye, Waziri Mkuu wa Poland, Mateusz Morawiecki, alibainisha kuwa nchi yake iko tayari kutoa usaidizi unaohitajika, ikiwa ni pamoja na timu ya uokoaji.

### MASHARIKI YA KATI

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alitangaza kwamba taifa hilo litatoa msaada wowote unaowezekana kwa Morocco, ikiwa ni pamoja na timu ya utafutaji na uokoaji, ikiwa Morocco itakuwa na hitaji hilo.

Pia Waziri Mkuu wa Iraq Mohamed al-Soudanim, alisema yuko tayari kutoa msaada wa aina yoyote, huku Mfalme Abdullah II wa Jordan akiagiza serikali yake kutoa msaada wote unaohitajika kwa Morocco, na kwamba Qatar nayo ilishatuma timu ya waokoaji.

### MASHIRIKA

Hata hivyo, inaelezwa kuwa Macron, mwishoni mwa mkutano wa G20 huko New Delhi, alitia saini na Waziri Mkuu wa India Narendra Modi, Rais wa Comoro Azali Assoumani, na viongozi wa Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa na tume ya Ulaya tamko la pamoja linaloahidi kutoa msaada wote muhimu kwa mahitaji ya haraka ya muda mfupi na juhudi za ujenzi upya.

Shirikisho la Kimataifa la mashirika ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu lenye makao yake Geneva lilitoa faranga milioni moja za Uswisi kutoka kwa hazina yake ya kukabiliana na maafa ya dharura ili kusaidia kazi ya hilali nyekundu ya Morocco katika shughuli ya utafutaji na uokoaji. **RFI**

# Idadi wanaotumia bangi Kenya yaongezeka

**NAIROBI,** Kenya

UTAFITI mpya wa mamlaka ya kitaifa ya kupambana na matumizi mabaya ya pombe na dawa za kulevya nchini Kenya (Nacada) unaonyesha kuwa matumizi ya mihadarati nchini humo yameibua wasiwasi mkubwa kuhusu kuenea kwa matumizi ya bangi miongoni mwa vijana wadogo.

Ripoti wa Nacada, ilibainisha kuwa idadi ya watu wanaotumia bangi nchini Kenya ilikaribia kuongezeka maradufu katika miaka mitano, ikielezwa kuwa takwimu mpya zinaonyesha mienendo ya kushangaza katika kuanza na kutumia dawa za kulevya.

Zinaonyesha kuwa umri wa chini wa kuanza kutumia vilevi mbalimbali ikiwa ni pamoja na tumbaku pombe na dawa za kulevya ni mdogo sana, huku hadi watoto wenye umri wa miaka sita wakiingizwa katika matumizi ya tumbaku.

Ilionekana pia kuwa matumizi ya dawa za kulevya kama vile heroni, huanza kutumiwa miongoni mwa watoto wenye umri mdogo kuanzia miaka minane na 18, wakati matumizi ya kokeini huanza katika umri wa miaka 20.

Ripoti hiyo iliangazia kuongezeka mara dufu kwa matumizi ya bangi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na hivyo kuibua wasiwasi kuhusu kuenea taarifa potofu na imani potofu zinazohusu madhara yake, hususani miongoni mwa vijana.

Takwimu zilizotolewa na Nacada zilizoainishwa katika ropoti ya kina, zinaelezea zaidi kuhusu uzito wa tatizo hilo. **BBC**



Wananchi wakiendelea kutafuta mali zao zilizofukiwa na vifusi baada ya makazi yao kuharibiwa na tetemeko la ardhi, katika eneo la Kusini Magharibi mwa mji wa kitalii wa Marrakech, Morocco, juzi. **PICHA: MTANDAO**

# ARTA SOLA7 YAANIKA TATIZO LA WASHAMBULIAJI AZAM FC

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Youssouf Dabo, amesema bado kuna kazi ya kufanya katika safu yake ya ushambuliaji ili kuweza kupata mabao mengi kwenye mechi za ushindani.

Azam FC juzi ilicheza mechi ya kirafiki ya kimatifa dhidi ya Arta Sola7 ya Djibouti na kuibuka na ushindi wa mabao 2-1, katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, ambao umemuonesha matundu Dabo katika safu yake ya ushambuliaji.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Dabo alisema bado anahitaji kupata michezo mingine ya kirafiki kwa kipindi ambacho hawatakuwa na ratiba ya mechi za Ligi Kuu Bara kwa ajili ya kufanyika kazi mapungufu aliyoyabaini.

**Alisema kikubwa ni kuwataka washambuliaji kuwa watulivu wanapokuwa kwenye eneo la mwisho la mpinzani na kuhakikisha wanatumia nafasi wanazotengeneza ili kupata ushindi wa mabao mengi.**

"Tumecheza mechi yetu ya kirafiki na kuona ubora wetu na madhaifu ambayo yako katika safu ya ushambuliaji hivyo tunaendelea kuwasisitizia kuwa makini na nafasi tunazotengeneza kuzitumia vema ili kupata mabao mengi katika mechi za ushindani," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa ligi imekuwa na ushindani mkubwa na kila timu inafanya maandalizi mazuri, hivyo wachezaji wanatakiwa kuwa makini uwanjani kwa kuhakikisha kila nafasi wanazotengeneza wanazitumia vizuri.

Alisema mwisho wa msimu nafasi hizo watazikumbuka kama malengo yao makubwa ya kutwaa mataji hayatatimia, hususan ubingwa wa Ligi Kuu ambao vigogo Simba na Yanga wanauhitaji kwa hamu.

Azam FC inatarajia kusafiri kuelekea Arusha kwa ajili ya mechi ya kirafiki wikiendi hii ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.




Wachezaji wa timu ya Kijitonyama Chipukizi katika picha ya pamoja wakifurahi na medali zao pamoja na hundi ya Sh. 600,000 waliyokabidhiwa baada ya kushinda mashindano ya Health Champions (Tanzania Champions Cup) yaliyoshirikisha jumla ya timu 24. **PICHA: PIGAPICHA WETU**

# Kijitonyama Chipukizi yatwaa ubingwa Health Champions

Na Mwandishi Wetu

TIMU ya Kijitonyama Chipukizi ya chini ya umri wa miaka 21 (U-21), imetwaa ubingwa wa mashindano ya Health Champions (Tanzania Champions Cup), yaliyoshirikisha jumla ya timu 24.

Kijitonyama Chipukizi iliishinda kwa penati 2-0 dhidi ya Moshi ya Buza katika mchezo wa fainali uliopigwa kwenye Uwanja wa Kijitonyama juzi baada ya dakika 90 kumalizika kwa suluhu.

Mchezo huo ulikuwa mkali na wa kusisimua ambapo kila timu ilikuwa inasaka ushindi kwa ajili ya kupata zawadi nono ambapo mwisho wa mchezo huo Kijitonyama Chipukizi ndiyo iliyoondoka na kitita cha Sh. 600,000, kombe na medali za dhahabu kwa kutwaa ubingwa huku mshindi wa pili Moshi Academy akizawadiwa Sh. 300,000 na medali za fedha.

Nafasi ya tatu ilikwenda kwa Madina ambayo iliifunga Young Stars na kuzawadiwa Sh. 200,000. Akizungumza baada ya mechi hiyo ya fainali, Kocha wa Kijitonyama Chipukizi, Frank Mnenga maarufu Didi, alisema wamefarijika sana kushinda zawadi hiyo na wachezaji wake wamepata hamasa zaidi.

"Nawapongeza wachezaji kwa kupambana muda wote, haikuwa kazi rahisi na zawadi hii ni kubwa tangu kuanzisha kituo chetu. Fedha hii pia itatusaidia kulipia gharama mbalimbali katika mashindano ya soka ya Ufukweni ya Shirikisho la Kandanda Tanzania (TFF)," alisema Didi.

Kocha wa Moshi Academy, Mohamed Makange, alisema pamoja na kushindwa kutwaa ubingwa, wameyafurahia mashindano kwani ni ya muda mfupi na yenye zawadi nono.

"Fedha tuliyoshinda itatusaidia kununua vifaa vya michezo na chakula kwani wachezaji wetu wanakaa kambini. Tumefurahi sana kushiriki mashindano yenye tija," alisema.

Mkurugenzi wa Green Sports Africa, George Ouma, alisema mashindano hayo yanafanyika kwenye nchi tano ikiwamo Tanzania. "Tanzania ni ya nne nchi nyingine ambazo zimefanya mashindano haya ni Uganda, Ghana na Nigeria. Nchi ya mwisho ni Senegal ambayo yatafanyika mwezi huu pia," alisema.

Alisema vijana wenye vipaji watakaopatikana kwenye mashindano hayo watapelekwa Marekani na Hispania ambako wataendelezwa vipaji vyao. Mkurugenzi mwenza wa Kampuni ya Green Sports Africa, Kassim Ismaili, alishukuru timu zote zilizoshiriki.

# Wavu Tanzania yawania 12-bora viwango Afrika

Saada Akida na Shufaa Lyimo

TIMU ya Taifa mpira wa Wavu Tanzania (Almasi Kings), kesho inashuka dimbani kusaka nafasi ya 12 katika viwango vya mchezo huo kwenye mashindano ya Afrika yanayoendelea jijini Cairo, Misri.

Almasi Kings iliyofanikiwa kufika hatua ya 16 bora katika mashindano hayo, inasubiri mshindi wa mchezo wa leo, Jumanne kati ya Mali na Burundi, watakayekutana naye kwa ajili ya kucheza nao kusaka nafasi hiyo ya 12 ya viwango vya Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alfredy Selengia, alisema wamefanikiwa kuingia hatua ya 16-bora, hivyo wanasubiri mshindi kati ya Mali na Burundi kwa ajili ya kucheza nao kutafuta nafasi ya 12 bora Afrika.

Alisema kulingana na timu yao kuwa changa, hatua hiyo waliyofika ni kubwa, hivyo watahakikisha wanapambana kufanya vizuri dhidi ya mpinzani yeyote watakayekutana naye kati ya Mali au Burundi.

"Kesho (leo), Mali na Burundi wanacheza tunapata wakati mzuri wa kuwaona wapinzani wetu, kwa upande wa Mali tulicheza nao mechi ya pili na kuwafunga seti 3-1, kwa maandalizi tuliyofanya ninaimani tutafanya vizuri katika mchezo wetu unaofuata na kuipandisha Tanzania katika nafasi ya 12 ya viwango vya Afrika," alisema Selengia.

Katika michezo ya awali timu hiyo ya Tanzania iliibuka na ushindi dhidi ya Timu ya Taifa ya Mali seti 3-1, Seti ya kwanza walishinda huku Seti mbili za mwanzo vijana wa Almasi Kings walitawala na kushinda Seti ya kwanza kwa pointi 18-25, Seti ya pili pointi 22-25 kisha Mali wakajiuliza kwenye Seti ya tatu na kuichukua pointi 25-17.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## DAVIES AWANIWA MADRID

REAL Madrid wanalenga kumnunua mlinzi wa Bayern Munich, Alphonso Davies, 22, msimu ujao wa majira ya joto. ***(Marca)***

## KLOPP AMTAKA AGUERD

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, anataka kumnunua mlinzi wa West Ham na Morocco, Nayef Aguerd, 27, msimu ujao lakini atakabiliwa na ushindani kutoka kwa Manchester City kwa mchezaji huyo. ***(Sun)***

## AIKATALIA NORWAY

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekataa nafasi ya kuinoa Timu ya Taifa ya Wanawake ya Norway. (Mirror)

## VERRATTI KATESA VIGOGO

CHELSEA, Barcelona na Bayern Munich zote zilijaribu kumsajili Marco Verratti, 30, kutoka Paris Saint-Germain msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Transfers)***

## HAG KUTETA NA SANCHO

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anatazamiwa kuzungumza na Jadon Sancho Jumatatu kwa mara ya kwanza tangu kocha huyo amshutumu winga huyo wa England kwa kutofanya vya kutosha kustahili nafasi katika kikosi cha kwanza cha klabu hiyo. ***(Telegraph)***

## VUSKOVIC KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur iko mbioni kumsajili beki wa Croatia, Luka Vuskovic, 16, ambaye alikuwa akihusishwa na kuhamia Liverpool, Chelsea, PSG na Manchester City, lakini mchezaji huyo hatajiunga na Spurs hadi msimu wa majira ya joto wa 2025. ***(Standard)***

## XAVI MKATABA MPYA

KOCHA wa Barcelona, Xavi anatazamiwa kutia saini mkataba mpya katika klabu hiyo wiki hii. ***(Fabrizio Romano)***

## BAENA AWANIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inataka kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Alex Baena, 22, kutoka klabu ya zamani ya kocha Unai Emery, Villarreal. ***(Fichajes)***

## PALHINHA AITAKA BAYERN

JOAO Palhinha ameitaarifu Fulham kwamba anataka kuondoka klabuni hapo Januari na kujiunga na Bayern Munich.***(Teamtalk)***

## BARELLA KUUZWA MWAKANI

INTER Milan ilikataa ombi la Chelsea, Liverpool na Newcastle United kwa kiungo wa kati wa Italia, Nicolo Barella, 26, msimu huu wa majira ya joto, lakini mchezaji huyo anaweza kupatikana kwa takribani pauni milioni 77 mwakani. ***(CaughtOffside)***

## MITOMA KUZUIWA CITY, LIVER

KLABU ya Brighton inataka nyota wake, Kaoru Mitoma abakie klabuni hapo kwa muda mrefu zaidi, wakati huu ambapo Man City na Liverpool zikimtolea macho. ***(Caughtoffside)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ANTONY YAMKUTA KAMA YA GREENWOOD UNITED

**MANCHESTER,** England

**Kama klabu tunalaani vitendo vya unyanyasaji, tunatambua umuhimu wa...**

MANCHESTER United na Antony wamekubaliana kwamba mshambuliaji huyo wa Brazil ataachwa nje ya klabu hiyo baada ya shutuma za unyanyasaji zilizotolewa na wanawake watatu.

**United ilitoa taarifa Jumapili kwamba Antony mwenye umri wa miaka 23, atachelewa kurejea mazoezini," ili kushughulikia madai hayo."**

Uamuzi huo ulitiwa saini na Mtendaji Mkuu wa Man United, Richard Arnold, baada ya mazungumzo na Kocha Erik ten Hag.

Madai yametolewa dhidi ya Antony na wanawake watatu tofauti, akiwamo mpenzi wake wa zamani Gabriela Cavallin.

Antony, ambaye alitemwa kwenye kikosi cha Brazil baada ya tuhuma mpya zilizotolewa na Cavallin, amekanusha makosa yote.

Taarifa ya United ilisema: "Manchester United inakiri tuhuma zilizotolewa dhidi ya Antony.

"Wachezaji ambao hawajashiriki mechi za kimataifa wanatarajiwa kurejea mazoezini Jumatatu (jana), hata hivyo, imekubaliwa na Antony kwamba atachelewa kurejea hadi itakapotangazwa tena ili kushughulikia tuhuma hizo.

"Kama klabu tunalaani vitendo vya unyanyasaji. Tunatambua umuhimu wa kuwalinda wale wote wanaohusika katika hali hii na tunakubali athari zinazotokana na tuhuma hizi kwa waathirika wa unyanyasaji."

Chanzo kimoja kimeiambia ESPN kwamba Antony, ambaye hajakamatwa au kufunguliwa mashtaka, hajasimamishwa kazi na muda wake wa kukaa nje unaelezewa kuwa ni "kupumzika" ili kuruhusu fowadi huyo kuzingatia kujilinda.

Anabaki kwenye malipo kamili na hakuna ratiba ya kurudi kwake. Madai yaliyotolewa dhidi ya Antony, ambaye alijiunga na United kutoka Ajax kwa pauni milioni 85 mwaka 2022, yanachunguzwa nchini Brazil na jijini Manchester.

Katika taarifa iliyotolewa na Antony Jumapili, ilisema: "Nimekubaliana na Manchester United kuchukua muda wa kutokuwapo wakati nikiwa nashughulikia tuhuma zilizotolewa dhidi yangu.

"Huu ulikuwa uamuzi wa pande zote ili kuepuka usumbufu kwa wachezaji wenzangu na mabishano yasiyo ya lazima kwa klabu.

"Nataka kusisitiza kutokuwa na hatia kwa mambo niliyotuhumiwa, na nitashirikiana kikamilifu na polisi kuwasaidia kufikia ukweli. Natarajia kurudi kucheza haraka iwezekanavyo."

Hivi karibuni mchezaji mwingine wa Man United, Mason Greenwood alikumbwa na tuhuma kama hizo na akasimamishwa kwa muda wa mwaka mzima, lakini baadaye hakupatina na hatia.

Lakini Man United imelazimika kumwondoa kikosini na sasa amepelekwa kwa mkopo Getafe ya Hispania ambapo atacheza kwa msimu mmoja.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
SCOTLAND
VERSUS
ENGLAND
1 | 4.02
X | 3.56
2 | 1.89

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA
MAOKOTO Deilee!
1. Nyalundi Nyalundi - 0654 645 XXX
2. John Mfilinge - 0656 564 XXX
3. Frank Chiganga - 0656 596 XXX
4. Basil Luiza- 0657 647 XXX
5. Frank Mkinga - 0657 729 XXX
6. Baraka Athmani - 0672 269 XXX
7. Juma Gwambiye - 0674 585 XXX
8. Moses Nanyaro - 0679 493 XXX
9. Sufiani Selemani - 0710 198 XXX
10. Abdul Milanzi - 0714 026 XXX
20,000/=
KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MO SALAH AVUTIWA KASI SAUDIA




**RIYADH,** Saudi Arabia

LICHA ya Klabu ya Al Ittihad kushindwa kumsajili Mohamed Salah kipindi cha dirisha la majira ya joto, lakini winga wa Al Khaleej, Fabio Martins, anaamini Mmisri huyo atakuwa kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia hivi karibuni.

Liverpool walikataa ofa iliyoripotiwa kuwa ya hadi pauni milioni 150 kwa ajili ya Salah, ambaye Jurgen Klopp alikuwa amedhamiria kutompoteza kwenye dirisha la usajili.

Inakisiwa kuwa Al Ittihad - ambao walimsajili Karim Benzema, Fabinho, Jota, Luiz Felipe na N'Golo Kante - watarejea na ofa nyingine kwa Salah katika kipindi cha miezi 12 ijayo.

Salah ni nyota wa dunia na Martins anatumaini kuwa hivi karibuni atapambana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31.

"Iwapo uhamisho huu utafanyika, atakuwa nyota mwingine mkubwa kuwasili hapa nchini," alisema Martins akiiambia Stats Perform katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Kucheza dhidi ya Salah kungekuwa jambo la kipekee pia. Haikufanyika wakati huu lakini nadhani katika soko lijalo la Januari, watajaribu kwa uhakika tena kumleta, na tuone kitakachotokea."



## Rais TFF ya Hispania hatimaye ajiuzul

**MADRID,** Hispania

LUIS Rubiales amejiuzulu kama rais wa Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), kwa sababu ya uchunguzi unaoendelea dhidi yake kufuatia kumbusu mdomoni mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake, Jenni Hermoso, bila ridhaa yake.

Hermoso aliwasilisha malalamiko ya jinai wiki iliyopita, ambayo yalisababisha waendesha mashtaka kuwasilisha kesi katika Mahakama Kuu ya Hispania dhidi ya Rubiales.

Anakabiliwa na mashtaka ya unyanyasaji wa kijinsia baada ya fainali ya Kombe la Dunia la Wanawake, ambapo Hispania ilishinda bao 1-0 dhidi ya England na kutwaa kombe hilo kwa mara ya kwanza.

Jumapili usiku, RFEF ilithibitisha kujiuzulu kwa Rubiales katika taarifa yake na kwamba atajiuzulu pia kama makamu wa rais wa Shirikisho la Vyama Vyama Soka Ulaya, UEFA.

Awali, Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), lilimsimamisha kufanya shughuli yoyote inayohusiana na soka kwa siku 90 huku likifanya uchunguzi wake lenyewe.

"Nimekabidhi kujiuzulu kwangu kwa kaimu rais, Pedro Rocha," Rubiales alitl tisha katika barua ya waz yochapishwa Jumapili.

"Pia nimemjulisha k nimefanya hivyo na na yangu kule UEFA ili kuta wa mbadala wa nafasi ya kama makamu wa rais.

"Baada ya kusimamis na FIFA, pamoja na zilizobaki dhidi yangu, wazi kuwa sitaweza kur kwenye nafasi yangu."

Huku kukiwa na hali n ya ya kisa hicho, kocha Hispania, Jorge Vilda aliti liwa Jumanne iliyopita.

Rubiales hapo awali al wa amekataa kujiuzulu l ya shinikizo hilo katika za hivi karibuni.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# SINGIDA KUTUMIA STAILI YA JKU KUIANGAMIZA FUTURE

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Singida Fountain Gate imesema itatumia staili ya upambanaji ya JKU ilivyocheza katika mechi ya mkondo wa pili ya Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi yao kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ili kupata ushindi dhidi ya Future FC ya Misri.

Jumapili wiki hii, Singida itashuka katika Uwanja wa Azam Complex, kucheza mechi ya raundi ya kwanza ya kombe hilo, baada ya kuiondosha JKU kwa jumla ya mabao 4-3 katika mechi ya hatua ya awali.

**Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hussein Massanza, alisema jana kuwa mbali na mifumo na mipango ya kocha wao mpya, Mjerumani Ernst Middendorp, lakini pia watatumia staili ya upambanaji walioionesha JKU katika mechi ya pili ya kombe hilo iliyopigwa Agosti 27, mwaka huu na kufanikiwa kuifunga Singida mabao 2-0.**

"Tunakwenda kucheza mechi ngumu dhidi ya Future ya Misri, tumejiandaa vizuri sana kiufundi na kimbinu chini ya kocha wetu, lakini tutaingiza staili ya upambanaji ya JKU walioionesha siku ile walipocheza na sisi.

"Tuwapongeze sana JKU siku ile walikuja kwa 'kujilipua', walikuwa hawana cha kupoteza, walikuja kucheza kwa kujituma wakitumia ule msemo wa 'liwalo na liwe', hii imetufundisha sana, tumepata somo kubwa sana kupitia JKU, tumechukua staili hiyo na sisi tutacheza dhidi ya Future, tunajua si saizi yetu kwa uzoefu na kila kitu, lakini na sisi itabidi 'tujilipue' kama JKU," alisema Massanza.

Alisema kupitia mechi ile pia wamejifunza kutomdharau mpinzani kwani walioshinda mabao 4-1 mechi ya kwanza Agosti 18 kwenye uwanja huo huo waliona kama wamemaliza, lakini kilichotokea hawakuamini na kukiri ilibaki kidogo wapindue meza kwani JKU ilihitaji bao moja tu ili kuzufu ambalo hawakubahatika kulipata.

Iwapo Singida watafanikiwa kuiondosha Future watatinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.




Msanii wa Muziki wa Singeli, Sholo Mwamba, akitumbuiza kwenye maonyesho ya wajasiriamali wanawake na vijana (IMBEJU), yaliyozinduliwa na Benki ya Crdb Foundation, katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Simba, Yanga Ligi Kuu kimeeleweka

INATOKA UKURASA 24

3, mwaka huu, ambapo sasa itachezwa Oktoba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Sababu ya mabadiliko hayo, bodi imesema ni Simba kuwa na mechi ya marudiano dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, Oktoba Mosi jijini Dar es Salaam.

## *Yanga 'kuiteka' Kigali*

INATOKA UKURASA 24

Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kikosi chao kimeingia kambini jana kwa wachezaji walikuwapo katika majukumu ya timu zao za taifa kasoro wachezaji wawili, Djigui Diarra na Stephane Aziz Ki.

Kuhusu msafara wa mashabiki kuelekea nchini humo, Kamwe alisema wamepokea taarifa kutoka matawi mbalimbali ya Dar es Salaam na mikoa mingine na hadi sasa takriban mabasi zaidi ya 50 tayari wamethibitishiwa kuwa yatakwenda nchini humo.

Alisema kwa Dar es Salaam tu jumla ya mabasi 13 yataondoka hapa Alhamisi kuelekea Kigali, Rwanda yakiwa yamejaa mashabiki na mengine yatatoka mikoa mingine tofauti kuelekea nchini humo.

Endapo Yanga itafuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, itakuwa ni mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 24 sasa.



## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 12/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 1935 | China vs Syrian Arab Republic | 1.96 | 3.49 | 3.81 |
| 15:20 | 5912 | Japan vs Turkey | 2.08 | 3.54 | 3.38 |
| 16:00 | 3328 | Kenya vs South Sudan | 1.72 | 3.53 | 5.16 |
| 16:00 | 4797 | Belarus U21 vs Portugal U21 | 15.31 | 7.35 | 1.11 |
| 16:30 | 1523 | Macedonia U21 vs Netherlands U21 | 8.13 | 5.28 | 1.27 |
| 18:00 | 2343 | Lithuania U21 vs Wales U21 | 4.47 | 3.76 | 1.64 |
| 18:00 | 5201 | South Africa vs DR Congo | 2.05 | 3.27 | 3.75 |
| 18:15 | 5826 | Qatar vs Russia | 2.96 | 3.22 | 2.43 |
| 19:00 | 3216 | Moldova U21 vs Georgia U21 | 3.47 | 3.42 | 1.93 |
| 19:00 | 3857 | Bulgaria U21 vs Israel U21 | 2.53 | 3.21 | 2.54 |
| 19:00 | 4736 | Azerbaijan vs Jordan | 1.88 | 3.43 | 4.22 |
| 19:00 | 5295 | Costa Rica vs United Arab Emirates | 2.03 | 3.43 | 3.64 |
| 19:30 | 3540 | Iceland U21 vs Czech Republic U21 | 2.86 | 3.26 | 2.25 |
| 19:30 | 3693 | South Korea vs Saudi Arabia | 2.12 | 3.43 | 3.37 |
| 19:30 | 5995 | Turkey U21 vs Italy U21 | 3.31 | 3.36 | 2.00 |
| 20:00 | 4562 | Kosovo U21 vs Germany U21 | 9.37 | 5.50 | 1.23 |
| 21:00 | 2778 | Peterborough vs Cambridge Utd | 1.70 | 3.67 | 4.18 |
| 21:00 | 4255 | Deportivo Coopsol vs Molinos EL Pirata FC | 1.22 | 5.25 | 9.90 |
| 21:30 | 2059 | Morocco vs Burkina Faso | 1.49 | 4.07 | 6.98 |
| 21:45 | 1076 | Spain vs Cyprus | 1.11 | 7.87 | 34.21 |
| 21:45 | 1251 | Coalville Town vs Redditch United | 1.94 | 3.81 | 3.10 |
| 21:45 | 1257 | Alvechurch vs Barwell | 2.09 | 3.61 | 2.90 |
| 21:45 | 1514 | Norway vs Georgia | 1.33 | 4.87 | 9.53 |
| 21:45 | 1791 | Switzerland vs Andorra | 1.07 | 9.48 | 42.13 |
| 21:45 | 1876 | Hendon vs Bracknell Town | 2.81 | 3.52 | 2.17 |
| 21:45 | 1984 | Italy vs Ukraine | 1.58 | 3.78 | 6.18 |
| 21:45 | 2062 | Leiston vs St Ives Town | 1.88 | 3.55 | 3.50 |
| 21:45 | 2090 | Leamington vs Berkhamsted FC | 1.78 | 3.41 | 4.07 |
| 21:45 | 2125 | Poole Town vs Gosport Borough | 2.54 | 3.61 | 2.33 |
| 21:45 | 2287 | Scotland vs England | 4.02 | 3.56 | 1.89 |
| 21:45 | 3152 | Stamford vs Stratford Town | 2.12 | 3.58 | 2.86 |
| 21:45 | 3437 | Malta vs North Macedonia | 4.95 | 3.58 | 1.73 |
| 21:45 | 3553 | Sweden vs Austria | 2.41 | 3.24 | 2.97 |
| 21:45 | 3701 | Israel vs Belarus | 1.41 | 4.53 | 7.59 |
| 21:45 | 4127 | AFC Sudbury vs Royston Town | 2.48 | 3.46 | 2.45 |
| 21:45 | 4248 | Romania vs Kosovo | 2.03 | 3.28 | 3.81 |
| 21:45 | 4527 | Swindon Supermarine vs Beaconsfield Sycob | 2.28 | 3.52 | 2.65 |
| 21:45 | 4544 | Belgium vs Estonia | 1.14 | 7.13 | 22.28 |
| 21:45 | 5032 | Telford vs Mickleover Sports | 2.59 | 3.51 | 2.33 |
| 21:45 | 5427 | Stourbridge vs Halesowen Town | 2.15 | 3.31 | 3.01 |
| 21:45 | 5893 | Kettering Town vs Needham Market | 2.79 | 3.60 | 2.15 |
| 21:45 | 5992 | Hungerford Town vs Dorchester Town | 2.23 | 3.47 | 2.76 |
| 22:00 | 1777 | Germany vs France | 2.89 | 3.46 | 2.36 |
| 22:00 | 2011 | Senegal vs Algeria | 2.07 | 3.22 | 3.75 |
| 22:00 | 3321 | Cameroon vs Burundi | 1.32 | 4.68 | 9.15 |
| 22:00 | 4233 | Ivory Coast vs Mali | 2.30 | 3.12 | 3.28 |
| 22:30 | 1371 | French Guiana vs Belize | 1.21 | 5.48 | 11.16 |
| 22:30 | 1677 | Saint Vincent and the Grenadines vs Bermuda | 3.01 | 3.21 | 2.19 |
| 23:00 | 5219 | Cuba vs Suriname | 2.81 | 3.06 | 2.40 |
| 23:00 | 5540 | Bolivia vs Argentina | 5.30 | 3.98 | 1.61 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Septemba 12, 2023

Nipashe




Mo Salah avutiwa kasi Saudia

UKURASA 22



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini kujiandaa na mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al-Merrikh itakayopigwa Uwanja wa Pele, Rwanda Jumamosi wiki hii. **PICHA: YANGA**

## Simba, Yanga Ligi Kuu kimeeleweka

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Bodi ya Ligi imetangaza rasmi kuwa mechi kati ya Simba dhidi ya Coastal Union itachezwa Septemba 21 saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Pia imetangaza tarehe za mechi zingine mbili, nazo ni Yanga dhidi ya Namungo na Azam dhidi ya Singida Fountain Gate.

Taarifa iliyotolewa jana na bodi hiyo imesema imetangaza tarehe ya mechi hizo baada ya awali kuwekwa kwenye ratiba, lakini hazikupangiwa tarehe kutokana na timu za Simba, Yanga, Azam na Singida kuwa kwenye michuano ya kimataifa.

Mechi ya Simba dhidi ya Coastal Union ndiyo ilikuwa gumzo kwani klabu hiyo iliiomba bodi kuipangia tarehe ya mapema kabla ya kucheza mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Power Dynamos kwa ajili ya kuwapa utimamu wa mwili wachezaji wake, lakini iligonga mwamba.

Mechi kati ya Yanga dhidi ya Namungo imepangwa kuchezwa, Septemba 20, saa 1:00 usiku katika Uwanja wa Azam Complex, huku Azam na Singida wakipangiwa kucheza Septemba 21, kwenye uwanja huo huo, saa 1:00 usiku.

Hata hivyo, Bodi imeweka angalizo kuwa kufanyika kwa mechi hizo pia kutategemea uthibitisho wa kuwapo au kutokuwapo kwa michezo ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambayo mpaka sasa, Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), halijatangaza terehe zake mpaka sasa.

Wakati huo huo, Bodi ya Ligi imetangaza kubadilisha tarehe ya mechi namba 29 kati ya Prisons dhidi ya Simba ambayo ilipangwa kuchezwa Oktoba

INAENDELEA UKURASA 23

# YANGA 'KUITEKA' KIGALI

## ●●● Mabasi 50 kubeba mashabiki, Gamondi achachawa akikumbusha 'mzimu' wa Al Hilal...

**Na Saada Akida**

WAKATI matokeo ya msimu uliopita ya kutolewa Ligi ya Mabingwa Afrika na Al Hilal ya Sudan yakimuumiza kichwa, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Angel Gamondi, mabasi takriban 50 imeelezwa tayari yamejaa kwa ajili ya kupeleka mashabiki wa Yanga jijini Kigali, Rwanda kwenda kuisapoti timu yao dhidi ya Al-Merrikh.

**Yanga ambayo msimu uliopita ilitolewa na Al Hilal katika mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, msimu huu inakutana tena na Al-Merrikh ya Sudan pia kwenye raundi ya kwanza, jambo ambalo Gamondi anataka kuandika rekodi ya kuwatoa Wasudan hao.**

Hata hivyo, tofauti na msimu uliopita ambao Yanga ilianzia nyumbani kabla ya biashara kwenda kuishia Sudan, msimu huu imepata bahati ya kuanzia ugenini na tena timu zote ni kama zipo ugenini kwani Al-Merrikh inachezea mechi zake za nyumbani nchini Rwanda kutokana na Sudan kuwa katika machafuko ya kisiasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi (pichani) alisema wanaendelea na maandalizi ya mwisho ya michezo ya hatua ya mtoano, anafahamu msimu uliopita walitolewa katika hatua kama hiyo na Al Hilal ya Sudan.



Alisema anajua ni muda mrefu Yanga haijacheza hatua ya makundi hali ambayo kuna ugumu lakini muhimu ni kuwa makini katika michezo miwili dhidi ya Al-Merrikh.

"Tumejipanga kuweka rekodi na historia mpya msimu huu, malengo yetu ni kuhakikisha tunafuzu makundi na kufika mbali zaidi kwani tunaamini kwenye ubora wa kikosi tulichonacho.

"Tunatakiwa kuwa makini na kuhakikisha tunashinda mechi zote mbili dhidi ya Al-Merrikh, ugenini na nyumbani ili tuendelee kusonga mbele na mashindano, tukipoteza hapa tutakuwa tumeaga mashindano jambo ambalo sitaki kuliona," alisema Gamondi.

Alisema amefanikiwa kuona baadhi ya video za mechi walizocheza Al-Merrikh na amefanyia kazi ubora na madhaifu ya wapinzani wao, hivyo anatambua utakuwa mchezo wa ushindani kwa sababu ya rekodi ya mechi ya msimu uliopita kutolewa na Al Hilal kutoka Sudan.

Wakati Gamondi akieleza hayo, Ofisa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >